Mji Utajengwa

Yeremia 31:38

"Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-kondoo. Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa mwenyezi Mungu; wenye utukufu wa Mungu"
Ufunuo 21: 9b - 11a

Tulipata msukumo wa kufikiri kuandika nakala hii kutoka kwa ndugu kutoka Colombia ambaye anaishi Australia, ambaye anajifundisha katika mafundisho ya kitume na huduma. Masomo mengi yametoka kwa habari za gazeti ambazo zimetolewa kwa miaka miwili iliyopita. Kila mara inatushangaza kuona vile Roho Mtakatifu anaongoza na kuwezesha. Mji utajenga! Huu ndio ufunuo unaoshikilia mafundisho yote katika nakala hii.

Paul Galligan
REVIVAL MINISTRIES AUSTRALIA

YALIYOMO

1. *Yesu na Bibi- arusi –una mapenzi na Yesu?* 3
2. *Mji utajengwa* 7
3. *Kanisa liko na misingi* 13
4. *Kuishi maisha ya utimilifu* 17
5. *Wakati kanisa linaomba* 21
6. *Hatua za utukufu* 26
7. *Mahali pa kudumu pa Mungu* 29
8. *Kanisa! ufalme!* 35
9. *Mitume – wajenzi wakuu* 39
10. *Thiologia ya kitume/Elimu ya kitume* 45

YESU NA BIBI-ARUSI

Uko na mapenzi na Yesu?

Katika waraka wake wa kwanza Petro anaandika ***"kwa wateule wa Utawanyiko, wakaao hali ya ugeni…kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mkapata kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo"*** **1Pet 1:1-2.** Petro hawaandikii 'watoto' tu lakini na mwili wa waamini. Na pia anawazungumzia kama "***watoto wachanga waliozaliwa"*** na anawaambia *"**yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu"*** **(2:2).**

Paulo anatukumbusha kwamba amekwisha ***"kutuposea mume mmoja"*** ili nimletee ***"Kristo bikira safi";*** anatuonya kinyume cha nyoka akitundanganya "***ili fikira zetu zisije zikaharibiwe, mkauache usafi wa unyofu na usafi wa Kristo"*** **(2 Kor 11:3).**

Wakati maziwa ni ya watoto na mwandishi wa ***Waebrania*** anawarudi kwa maana "***nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu"*** **(5:12*),*** kuna uhakika ambapo sisi wote tunahitaji kupokea na kukaa tukiwa na mtazamo wa *upendo wa kwanza* (**Ufu 2:4).** Tunahitajika kuja katika ule wepesi wa Yesu, mwokozi wetu, mkombozi wetu na kuwa na mapenzi na yeye mara na mara tena.

Mungu alimwambia Yeremia amuite kwa maana Mungu alitaka kufunua kwa Yeremia moyo wake wa urejesho wa watu wake, ambao wangekuwa Bibi-arusi wake.

Niite mimi

Mungu alisema kwa Yeremia wakati alipokuwa gerezani, ***"niite, nami nitakuitika, nami nitakuonyesha mambo makubwa magumu usiyoyajua"*** **Yer 33:3.**

Neno 'wita' ni neno la nguvu la kiebrania linalomaanisha '*kumuita mtu, kulia, kumuongelesha mtu, kupasa sauti, kunena, kutangaza*'. Neno 'Makuu' inaweza pia kumaanisha '*yasioweza kufikika'.* Ambayo Mungu anataka tuyajue yanawezekana tu akiyafunua kwetu. BWANA [MIMI NDIYE] kisha anamwambia Yeremia baadhi ya mambo ya ajabu ambayo ameahidi kuyatenda **(aya 4-16)** katika ***"habari za nyumba ya Israeli, na katika habari za nyumba ya Yuda"*** **Aya 14.**

Wingi wa kweli

Mungu alimwambia Yeremia kwamba nyumba zile ***"za Wafame wa Yuda, zilizobomolewa ili kuyapinga maboma na upanga"*** yatajengwa tena **aya 4, 5, 7.** Aliahidi ***"afya na kupona".*** Alisema ***"nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na kweli"*** **(aya 6).**

Kupatikana waaminifu

Katika maombi yanayoendelea katika SHILOH juzi, maneno mawili yenye nguvu ya hekima yameachiliwa kwetu. Ya kwanza ni **Mungu haangalii wahuduma waliofaulu, lakini wale waaminifu'.** Tumejifundisha maandiko kuhusu kuaminika na kuwa waaminifu. Katika **Yn 17:4**, Yesu alisema kwa Baba yake, ***"mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye".*** Yesu anazungumzia huduma yake ya kitume katika kuiweka kanisa kwa kuwachagua na kuwainua wale mitume kumi na wawili na pia kutambua kwa mmoja alikuwa ni mwana wa upotevu. Yesu aliaminika katika kuyatenda tu yale aliamuriwa na Baba kutenda; alikuwa ***"mwaminifu kwake yeye aliyemweka"*** **(Ebr 3:2).** Paulo anatuambia, ***"hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu"*** **1Kor 4:2.**

Kuongea ukweli katika upendo

Neno la pili la hekima lilikuwa 'haijatosha kutumaini uhusiano; kuna haja ya uaminifu'. Kumekuwa himizo nyingi katika uhusiano wa urejesho wa kitume lakini wakati mwingine katika gharama ya ***"tuishike kweli katika upendo"*** **(Efe 4:15)**. Hii ndio njia pekee tu ambayo ***"tutakua hata tumfikie yeye katika yote, aliye kichwa, Kristo".*** Kutoongea ukweli inaelekeza kuanguka katika uhusiano! Mungu ameahidi **kufunua wingi wa amani.**

Kuondolewa kwa dhambi – msingi wa urejesho

Mungu alimuahidi Yeremia kwamba kutakuwa na **urejesho: "***wafungwa wa Yuda, na wafungwa wa Israeli"* watarejea na kujenga upya (**Yer 33:7).**

Urejesho unaweza tu kutekelezwa wakati watu wa Mungu **wamemrudia BWANA kikamilifu.** Kutubu inaelekeza kwa msamaha na Mungu alisema, ***"nami nitawasafisha na uovu wao wote, ambao kwa huo wamenitenda dhambi; nami nitawasamehe maovu yao yote, ambayo kwayo wamenitenda dhambi, na kukosa juu yangu"*** **(aya 8).**

Watu waliorejeshwa watakuwa kwa Bwana Yesu, ***"jina la furaha, na sifa na utukufu, mbele ya mataifa yote ya dunia, watakaosikia habari ya mema yote niwatendeayo*** **[**watu wa Mungu]***"*** **aya 9.**

Mungu anawainua watu, hata kama ni mabaki, ambao watadhihirisha ***"utajiri wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27.**

Mazao ya urejesho

"Itasikika tena sauti ya furaha na sauti ya shangwe, sauti ya bwana arusi na sauti ya bibi arusi" **(Yer 33:10-11).** Kusudi la Mungu la milele limehakikishwa kutimizwa: tayari ***"Kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** **(Efe 3:11).** Kutakuwa na kudhihirishwa kwa kanisa kamilifu duniani!

"Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa, vyote vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu" **Rum 8:22, 19.**

Yesu mwenyewe "***analitakasa na kulisafisha kanisa kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** **(Efe 5:26–27).**

Kumuandaa bibi- arusi

Ujumbe wa kanisa bibi-arusi akiandaliwa hapa duniani pole pole inaruhusu dhamili zetu za kiroho! **Sauti ya bwana-arusi inasikika! Bibi-arusi anajiweka tayari.**

Uhusiana wa bibi/bwana arusi wazi unazungumzia kuingiana. Twahitaji kusikia ***"sauti ndogo ya utulivu"*** **(1Wafalme 19:12).** Twahitajika kuwa makini jinsi ya kumwendea na tusiseme ***"nimeivua kanzu yangu; niivaeje"*** **(Wimbo ulio bora 5:3).**

Tunatakiwa kupatikana miongoni mwa wale wanawali watano wenye hekima **(Mat 25:1-13),** tukiandaliwa na tayari kwa kuja kwa Bwana arusi. Funguo za hekima kwa wale wanawali watano ilikuwa kujiandaa na mafuta ya kutosha. Mafuta yanaongea juu ya upako wa Roho Mtakatifu; unazungumzia uhusiano wa karibu na Yesu tunapongojea kuja Kwake.

Wachungaji wa kweli

Ahadi ya Yeremia ambayo inahakikisha kuhusishwa kwetu katika kanisa huyu bibi-arusi ni kwamba "***yatakuwapo makao ya wachungaji wakizilaza kondoo zao. Makundi ya kondoo yatapita tena chini ya mikono yake awahesabuye"*** **Yer 33:12b, 13b.**

Ni wakati tutakapojipata katika uhusiano wa kujipatiana katika mwili wa Kristo, katika vikundi vya kitume ambapo Mungu ametuweka, ambapo tutapata uhusiano huu wa ndani na Yesu. Tena katika siku zetu, Mungu anawainua wachungaji ambao wana moyo wake. Anawapa "***wachungaji wanipendezao moyo wangu, watakaowalisha kwa maarifa ya fahamu"*** **Yer 3:15.**

Mfalme anapewa jina

Kilele cha ahadi ya Mungu kwa Yeremia kwa mabaki ambayo yanarejeshwa yanakuja katika **Yer 33:15-16**. Katika **Yer 23: 5-6**, Mungu tayari ameahidi kuinua kwa Daudi ***"chipukizi la haki: naye atamiliki mfalme, atatenda kwa hekima naye atafanya hukumu na haki katika nchi. Katika siku zake Yuda ataokolewa, na Israeli atakaa salama; na jina lake atakalo itwa ni hili: YHWH Tsidekenu – BWANA ni haki yetu".*** Huyu hawezi kuwa mwingine ila Bwana Yesu Kristo. Yeye ndiye BWANA haki Yetu.

Kanisa linapewa jina lilo hilo

Katika **Yer 33:15** inarudia **Yer 23:5**, lakini katika **aya 16**, ni bibi-arusi ambaye anapewa jina lile lile: ***"ataitwa YHWH Tsidekenu".***

Kanisa (bibi-arusi) anatakiwa kuitwa **YHWH Tsidekenu**. Kanisa (bibi-arusi) amewekewa hatima kuchukua jina la Bwana arusi!! Jinsi ilivyo ya kustajaabisha!

Yesu anaandaa bibi-arusi Wake, je unaandaliwa?

Uhusiano wako na Yesu uko namna gani?

'*Ninazidi kuingia kwa mapenzi na yeye mara kwa mara'.* Unaweza kuimba wimbo kama huo? Uhusiano wako na Yesu uko namna gani?

Njia za kuangalia uhusiano wako na Yesu ni:

- Huwa unaongea kuhusu Yesu?
- Huwa unaongea na Yesu?
- Huwa unaimba sifa na ibada kwake?
- Una shukrani?
- Unatembea katika uhusiano wa karibu na Yesu?
- Unanyenyekea kwa Yesu na hivyo kunyenyekea kwa wandugu?

Yesu ametujaza na Roho wake ili tutembee na uhusiano wa karibu naye, tukipata ujuzi wa pendo lake "***likisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"*** **Rum 5:5.**

Maisha yaliojaa Roho yanaambatana na mambo matatu kama sio manne, ambayo yanatambulika: **Efe 5:18-21.**

i. ***"Msilewe kwa mvinyo"*** **–** sio kuangalia kutimizwa katika raha za dunia bali ***"mjazwe Roho";***

ii. ***"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu";***

iii. ***"na kumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo";***

iv. *"**hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo".***

Kama tukitembea kwa uhusiano wa karibu na Yesu, tukiishi maisha yaliojaa Roho Mtakatifu hakika tutakuwa na furaha na kuwa furaha kwa wale walio karibu nasi. Watu kama hao watawavuta kwa urahisi watu kwa Yesu. Watu kama hao watahimiza wale walio karibu nao kurejelea na kuzifanya kazi za kwanza ili tutambue upendo wetu wa kwanza kwa Yesu, na kuwa makini kwake anapotukaribia.

MJI UTAJENGWA

"*Tazama, siku zinakuja, asema BWANA, mji huu utakapojengwa kwa ajili ya BWANA, toka buruji ya Hananeli hata lango la pembeni"* Yer 31:38.

Mungu ameahidi na hatagaili: **Mji wa Mungu utajengwa.** Huu ndio mji ule ule ambao Ibrrahimu aliona katika maono: ***"maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu"* Ebr 11:10.**

Yohana aliuona mji huu: ***"nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe"* ufu 21:2.** Jambo lililo kubwa kuhusu mji huu ni kwamba Mungu yuko katikati yake: ***"tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita"* ufu 21:3-4.**

Mmoja wa wale malaika saba akaja kwa Yohana akasema, ***"Njoo huku, nami nitakuonyesha Yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-kondoo. Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa mwenyezi Mungu, wenye utukufu wa Mungu"* ufu 21:9b -11a.**

Tumeufikilia mji huu tayari: ***"bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni"* Ebr 12:22-23a.**

KANISA ALIYE-BIBI ARUSI NDIYE MJI!

Mji huu unaweza kujengwa aje? ***"Tazama, mimi ni Yahweh, Mungu wa wote wenye mwili; je! kuna neno gumu lo lote nisiloliweza?" Yer 32:27.*** Yeremia alimjua Mungu, ***"Aa! Bwana Mungu (Adonai) Yahweh! tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyoshwa; hapana neno lililo gumu usiloliweza"* Yer 32:17.**

Sura 30 mpaka **33** ya **Yeremia** imejaa ahadi za ajabu na ukuu ambazo Mungu amezifanya. Katikati mwa sura hizi za urejesho na kudhihirishwa kwa siri za Mungu, Yeremia alitabiri, ***"kwa maana Yahweh ameumba jambo jipya duniani; mwanamke atamlinda mwanamume"* Yer 31:22**.

Kwanza ukisoma mambo haya inaonekana haina maana. Mungu alimuumba mwamamme na mwanamke mwanzo wawe mmoja, lakini Yeremia anatabiri kwamba Mungu anaumba jambo jipya. Yale alidhihirisha katika kumuumba Adamu na Hawa na kuwawezesha kuwa mmoja, atayatimiza kwa kuumba kanisa aliye bibi-arusi kwake, kwa mwana wake, Yesu Kristo.

Katika **Efe 5:22-33**, Paulo anafundisha kuhusu ndoa lakini katika kuyatenda hayo, hakika anafundisha kuhusu kanisa aliye bibi arusi. Anasema, ***"siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya kristo na kanisa"* aya 32.**

Uhusiano ni upi kati ya Masihi Yesu na kanisa lake?

Katika kitabu cha **waefeso 5**, mtume anatuagiza jinsi ya kujitayarisha kufanyika kanisa aliye bibi arusi na kisha anaorodhesha jinsi Kristo ndiye Bwana Mume ambaye anatuandaa tuwe kanisa aliye bibi arusi. Maagizo yamewekwa kwetu kama ***"watoto wanaopendwa"*** **Efe 5:1.** Kama tunapotembea kwa uaminifu katika kutimizwa kwa maagizo ya maaelekezo ambayo Paulo anatupa, tutakuwa ndani ya Kristo kufanyika kuwa sehemu ya bibi arusi wake. Jambo kuu ni ***"mfuateni Mungu"*** **aya 1.** Jambo la pekee ambalo tunaweza kuwa bibi arusi ni kufuata Mungu – tufanyike kama yeye. Kumbuka ya kuwa mwanzo Mungu alituumba kwa sura yake, kulingana na mfano wake.

Hata hivyo, kanisa bibi arusi atakuwa ***"mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **(Efe 4:13b).** Msidanganyike! Jambo lililopungua utimilifu kamili sio bibi arusi.

Tembea katika upendo

Twatakiwa kuwa na mapenzi na Yule atakaye kuwa mume wetu. Wakati mtu ana mapenzi na mwingine, anafuatilia huyo; tunatamani kuwa katika kikundi chao; tunazibeba kumbukumbu za huyo mtu. Wakati mwingine tukiwa wachanga, kama watoto wanapokua, 'tunajipata tumevunjwa' au kufutwa kwa wengine. Sio vibaya kuwa na hisia kama hizo kwa Yesu, lakini tunapaswa kukua kupita hatua ya kupendezwa na hisia, kuwa makini kuhusu kuendeleza uhusiano wetu na kuwa waaminifu katika uhusiano huo.

Katika mazingira, Paulo anaonya kinyume ***"uasherati na uchafu wote au kutamani…wala aibu, na mengineyo"*** **(Efe 5:3-4).** Hatuwezi kuwa sehemu ya kanisa aliye bibi arusi tukiwa na sehemu na mambo kama hayo – wandugu haya yanamaanisha ni lazima tutawale ambacho unaona katika runinga.

Hii inamaanisha kwamba tuyaache yote tuliojipatiana kwayo kwa 'kanisa' na kujipatiana kikamilifu kwake. Hatustahili kundanganywa na **"*maneno yasio na maana"* (aya 6),** au ***"tushirikiane na wana wa uasi"*** **(aya 7).**

Kutembea kama wana wa nuru

Kumbuka ya kuwa Paulo anatuagiza jinsi ya kujiandaa kwa arusi. Tunapaswa "***kutoshirikiana na matendo yasiozaa ya giza"*** **(aya 11).** Hata hatupaswi kuongea **"*yanayotendeka kwao kwa siri"* (aya 12).**

Matunda ya kutembea katika nuru ni "***wema wote na haki na kweli" aya 9.*** Jambo kuu katika haki ni imani na ukweli ni neno. Wema ni tunda la Roho katika maisha yetu (**Gal 5:22).** Tunapaswa kutafuta "***ni nini impendezayo Bwana"*** **(aya 10).** Kama tukitembea kama wana wa nuru, tunatembea katika mchana; tunahitaji kutojikwaa.

Ni wakati wa kuamka! Kanisa kwa jumla limelala! Tumekuwa katika msingi wa kulala na mafundisho ya elimu ya dunia iliyo wekwa maji. Kanisa katika jamii halionekani kama bibi arusi anayejiandaa kwa ajili ya Yesu, lakini zaidi na zaidi ni kanisa kahaba, anayechukua na kutenda njia za dunia.

Isaya ametuita ***"ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa BWANA umekuzukia"*** **Isaya 60:1.** ***Amaka wewe usinziaye, ufufuke katika wafu, na Kristo atakuangaza"*** **Efe 5:14.**

Tembea katika hekima

Maandiko yanasema, ***"angalieni sana jinsi mnavyoenenda, si kama watu wasio na hekima, bali kama watu wenye hekima"*** **Efe 5:15.** Tunahitaji kutafuta hekima katika kila hali. Tunahitaji kuangalia mambo na tusindanganyike kama wapumbavu, ***"mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu" aya 16.*** Tunapaswa ***"kufahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana"*** **aya 17.** Wakristo wengi wanaohudhulia kanisa hawajafahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Mungu. Wahubiri wengi wanaohubiri makanisani hawahubiri maarifa ya mapenzi ya Mungu. Wanahubiri mafundisho ya wanadamu na utafsiri wa wanadamu. Hekima tunayohitaji ni hekima itokayo juu (**Yakobo 3:1).**

Maisha yaliyojaa Roho

Tunahitaji kujazwa na Roho. Hatupaswi kuangalia kutosheleka katika raha za dunia kama ulevi. Maisha yaliyojaa Roho imefuatana na mambo matatu ambayo ni tofauti:

- Kusemezana mmoja na mwingine kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni (**aya 19**).
- Mkiwa na nia yenye shukrani (**aya 20**).
- Mkinyenyekeana mmoja na mwingine ***"katika kicho cha Kristo"*** **(aya 21).**

Bibi arusi amejaa Roho. Ni "***Roho na bibi arusi wasema njoo!" Ufu 22:17,*** wakati kanisa liko tayari kumpokea mume wake, Kristo Yesu.

Huku ni kujiandaa kwetu kama "***watoto wanaopendwa" Efe 5:1*** kuweza kukua katika Kristo kuwa kanisa bibi arusi wake.

Yesu ni nani na jinsi anajiandaa kumpokea bibi arusi wake – Efe 5:22- 32

i. Yesu ndiye kichwa cha kanisa (**aya 23**). Je wewe ni mshiriki?

ii. Yesu ndiye mwokozi wa mwili (**aya 23**). Umeokoka?

iii. Kanisa linapaswa kutii Kristo katika kila jambo (**aya 24**). Unamtii Kristo, au unajifurahisha wewe mwenyewe?

iv. Yesu analipenda kanisa (**aya 25**). Unatambua upendo wake kwako?

v. Yesu alijitoa kwa ajili ya kanisa (**aya 25**). Alilipa gharama kwa ajili ya kila mmoja apate kuokolewa.

vi. Yesu analitakasa kanisa, hivyo ni, kumweka wakfu kwa ajili yake (**aya 26**). Maisha yako yametengwa kwa ajili ya Mungu?

vii. Yesu analitakasa kanisa kutoka dhambi zote (**aya 26**). Umewekwa huru kutoka kwa dhambi? Yesu anatakasa na Yesu analiosha kanisa ***"kwa maji katika neno".*** Hili ni neno lililo huishwa la Mungu, je huwa unalipokea neno lililo huishwa?

viii. Yesu atajiletea kanisa tukufu (**aya 27**). Hili ni kanisa linalotembea katika ufunuo wa utukufu wa Mungu; kanisa linalojua ***"Kristo ndani yetu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27.** Hii ni kazi ya huduma: kufanya zijulikane siri za utukufu wa Mungu. Umezijua siri?

ix. Yesu anatupenda kama anavyojipenda (**aya 28**). Huu ni upendo unaotufunika! Una uhusiano wa ndani na Yesu?

x. Yesu analisha na kutunza kanisa (**aya 29**).

xi. Sisi tu washiriki wa mwili wake, ***"tu viungo vya mwili wake"*** **(aya 30).** Sisi tu mmoja naye: tunapaswa kumkaribia jinsi gani!

xii. Kuna kuacha (ya kale) na kuambatana na Yesu, kuwa mmoja na yeye (**aya 31**).

"siri hiyo ni kubwa; Ila mimi na nena habari ya Kristo na kanisa"

Yeremia alizungumza kuhusu urejesho huu mkuu – Yer 31:1-14

"Wakati huo, asema Yahweh, nitakuwa Mungu wa jamaa zote za Israeli, nao watakuwa watu wangu" Yer 31:1. Petro alisema kwamba "***ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema"*** **1Pet 2:10.** Mungu aliahidi ya kuwa kupitia Ibrahimu "***jamaa zote wa dunia watabarikiwa"*** **Mwa 12:3.** Yeremia anawazungumzia Waisraeli lakini kwa hakika Israeli hawakuwapo katika asili wakati huo. Ufalme wa Israeli ulikuwa umepotea na watu wa Israeli walikuwa wametapanyika. Ni ufalme wa Yuda tu uliokuwa umebaki. Katika kuzungumza kuhusu Israeli maandiko yanakamata picha ya urejesho wa watu wote, Wayahudi na watu wa mataifa, kuwa Israeli mpya ya Mungu (**Gal 6:16**). Mungu ni Mungu wa jamii zote za dunia na atakuwa na watu wateule watakaokuwa mji wake.

Kupatikana kwa neema

Aya 2 Watu hawa walikuwa wamepotea jangwani; watu hawa walikuwa wamepitia hukumu kali, lakini walipata ***"neema jangwani".*** Mara tumepatikana kwa neema, hivyo ni, kuokolewa ndani na kupitia Yesu Kristo, Mungu anataka kutuleta pahali pa raha (**Ebr 4:3**). Hatimaye pahali pa raha ya Mungu ni mji wa mbinguni ambao unaitwa mlima Sayuni ama Yerusalemu katika **Ebr 12:22**. Mji huu ni mji wa kiroho na tayari tumeufikilia.

Kuvutwa kwa upendo

Aya 3 Yahweh anasema, ***"nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu".*** Mungu anatupenda na kutoka kwa upendo wake ametuita.

Urejesho unaleta furaha

Aya 4 urejesho umeanza kufanyika. Wajibu wa huduma ni 'kujenga'. Katika kupaa kwake, Yesu amepeana karama za huduma tano ***"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata mwili wa Kristo ujengwe hata kufika… mtu mkamilifu"*** **Efe 4:11-16.** Sehemu ya maagizo ya Mungu kwa **Yeremia** katika sura ya **1:10** ilikuwa ***"kujenga na kupanda".*** Kuna kujenga upya wa kile ambacho '***kimeng'olewa na kubomolewa'.*** Nyumba inajengwa ya Kristo kuishi.

Kuna kufurahia pia! Bibi arusi bikira anaandaliwa tayari kwa ndoa. Hiki ndicho kilele cha kujenga mji.

Mazao

Aya 5 Mara urejesho umetendeka kutakuwa na mazao. Katika kanisa, wengi wetu wamekuwa wakiomboleza kwa ukosefu wa mazao lakini katika siku hizi, wale watu wamepata ujuzi wa urejesho wa kitume wanaona mazao ambayo yanadumu (**Yn 15:16**).

Hebu na tuende Sayuni

Aya 6 Walinzi wa kinabii (waombezi) wana jukumu kuu la kutekeleza katika urejesho na kujenga tena mji. Mungu anasema, ***"nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku, ninyi wenye kumkubusha Yahweh msiwe na kimya; wala msimuache akae kimya mpaka atakapoufanya imara Yerusalemu, na kuufanya kuwa sifa duniani"*** **Isaya 62:6-7.** Siku imekuja kwa walinzi kusema kwa Efraimu.

Efraimu aliwakilisha ufalme wa kaskasini ambao walipotea katika historia. Mungu anasema kiunabii ya kuwa walinzi katika mlima wa Efraimu watasema, 'hebu na tuinuke, sio kukaa hapa na kuenenda katika Sayuni'. Efraimu anawakilisha watu wa Mungu ambao

wamekuwa vuguvugu, walioanguka. Hawa ndio ambao Mungu anaita ili wainuke 'toka; usikae katika hali yako ya kuanguka'.

Watu wanaitwa waje Sayuni. ***"Na mataifa mengi watakwenda na kusema, 'Njoni, twende juu mlimani kwa Yahweh, nyumbani kwa Mungu wa yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake'; maana katika Sayuni itatoka sheria; na neno la Yahweh katika Yerusalemu"*** **Isaya 2:3.** Kama tukikaa katika Efraimu, hatutaufikia Sayuni.

Sikia neno la kiunabii: ***"Inukeni, tukaende Sayuni, kwa Yahweh, Mungu wetu"*** **Yer 31:6b.** Ni wakati wa kutodumu mahali ambako umekuwa; ni wakati wa kutoka; ni wakati wa kuwa tayari kuolewa na Yesu.

Wokovu wa watu

Aya 7 Watu watakuja kwa kuimba, furaha na sifa. Yakobo atafanyika Israeli. Yakobo alikuwa ni mtu aliyesubuka na shinda zake; alimenyana na Mungu na akapokea ufunuo wa kuwa Mungu ni nani- ufunuo huu ulimbadilisha daima. Akawa mtu mpya na jina jipya – Israeli (**Mwa 32:28-29**).

Watu watalia ***"Oh Yahweh, waokoe watu wako".*** Kilio hiki kilisikika Yerusalemu wakati Yesu aliingia mjini jumapili ya mitende, ***"Hosana! Ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana, Mfalme wa Israeli"*** **Yn 12:13.** (Hosana inamaanisha *okoa sasa*!)

Petro anatuambia kama waamini tuweke mbali "***uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote. Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu"*** **1Pet 2:1-2.** Hata kama wakristo waliokomaa tunapaswa kuhifadhi usafi wa uhusiano wetu na Yesu.

Kikundi kikubwa kitakuja

Aya 8 Mungu atawakusanya wanyonge; vipofu, wachechemeao, mwanamke mwenye mimba, jeshi kubwa. ***"Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia…mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu"*** **1Kor 1:26-29.**

Pokea urithi wa wazaliwa wa kwanza

Aya 9 Watakuja kwa kulia – kulia inazungumza juu ya unyenyekevu, tukifahamu hatujafika – na dua, kumlilia Mungu. Kama matokeo Mungu ***"atawaendesha penye mito ya maji katika njia iliyonyoka; katika njia hiyo hawatajikwaa".*** Ahadi ya ajabu namna gani! Kama tukinyenyekea na tuanze kumtafuta Mungu kwa bidii, atahakikisha tumepata mito ya maji; ya kuwa tutatembea katika njia zilizonyoka (njia nyembamba).

Mungu ni Baba kwa Efraimu. Yeye anakusudia watu wake wote wafanyike wana. Anawaita Efraimu ***"mzaliwa wangu wa kwanza!"*** Mzaliwa wa kwanza anapokea urithi. Kanisa la kweli ni la wana wazaliwa wa kwanza (**Ebr12:23).** Kila mtu anaye mwamini Yesu amezaliwa tena kuwa mtoto wake na kuwekewa hatima yake kukua na kurithi, kwa kuwa kila mtoto wa Mungu ana haki ya mzaliwa wa Kwanza?

Mchungaji kwa watu wake

Aya 10 Mungu atawakusanya pamoja watu wake na kuwaweka ***"kama mchungaji alindavyo kundi lake".*** Yesu alisema, ***"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema hutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo"*** **Yn 10:11.**

Kukombolewa na kuwekwa huru

Aya 11 Watu wanakombolewa na kuwekwa huru na BWANA. Yesu aliharibu ***"yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa"*** **Ebr 2:14-15.**

Nafsi zinarejeshwa

Aya 12 Njoo na uimbe katika maeneo yaliyoinuka ya Sayuni. ***"Tembeeni katika Sayuni, uzungukeni mji, Ihesabuni minara yake, Tieni moyoni boma zake, Yafikirini majumba yake, Mpate kuwaambia kizazi kitakachokuja"*** **Zab 48: 12-13.** Sayuni ni pahali pa ajabu ndani ya Mungu: anatualika tuangalie katika kila chumba, kutafuta utajiri wake – kila kitu katika Sayuni kinatiririka uzuri. Kupatikana kwa mavuno kupo. Nafaka –mkate wa neno; divai mpya- furaha ya Roho; mafuta – upako wa Mungu.

"Na roho zao zitakuwa kama bustani iliyotiwa maji; wala hawatahuzunika tena kabisa". Hapa ni pahali pa burudani ya nafsi; jifunze kukaa katika bustani na Yesu; ruhusu maji ya neno yakuoshe; mruhusu akuburudishe na arejeshe roho yako na alete uponyaji kwa roho yako. Mungu anataka kutuponya na kutuachilia kutoka kwa huzuni. Wengi wetu hubeba huzuni za kale lakini Yesu "***amejitwika huzuni zetu… adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona"*** **(Isaya 53:4-5).**

Maisha ya kiroho yatatiririka. ***"Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake"*** **Yn 7:38.** Isaya anasema, ***"kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu"*** **(Isaya 12:3**).

Kujazwa na utimilifu wote wa Mungu

Aya 13-14 Kutakuwa na kushangilia na kufurahia. Watu 'watakuwa wamejazwa kabisa' na kutoshereka kabisa na kujawa na utele. Watu watalidhika na wema wa Mungu ***"na kuujua upendo wake Kristo upitao ufahamu… mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"*** **Efe 3:19.**

Agano jipya – Yeremia 31:31-34

Ahadi hizi zote za ajabu zinawezekana na zitatimizwa kwa sababu ya agano jipya, ambayo Mungu aliahidi katika sura hiyo hiyo ya Yeremia. Mungu anajiona kama mume kwa watu wake; hata katika agano la kale alisema, ***"ingawa nilikuwa mume kwao"*** **(aya 32b*).***

Siku inakuja wakati kanisa litarejeshwa! Mji utajengwa! Wote watamjua Yahweh, hivyo ni, wote watamjua Mungu kupitia uhusiano wa kibinafsi, na upendo wa kujitolea, kwa Yesu Kristo.

"Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika;
nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu ...
watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao
hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema BWANA.
Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena".
Amen.

KANISA LINA MISINGI

Kazi kubwa ya mtume ni kuiangalia misingi, kuiweka nguvu misingi na, kwa hali zingine, kuweka upya misingi. Mtume anatakiwa kuwa ***"mkuu wa wajenzi mwenye hekima"*** **(1Kor 3:10);** yule mwenye uweza wa kuelekeza ujenzi wa Nyumba ya Mungu. Nyumba ni ya Yesu aliye Kristo **(Ebr 3:6**), na sisi watu wa Mungu ndio nyumba, tukiungamanishwa kama mawe yaliyo hai kwake (**1Pet 2:5**).

Kila nyumba itakayo thibiti mateso na majaribio yatakikana kujengwa juu ya msingi wa pekee wa kweli, ambao ni Yesu aliye Kristo (**1 Kor 3:11**), na kujengwa sawa sawa na neno lake, sio tamaduni za wanadamu, iwe hiyo tamaduni ni ya wakatoleki wa Kirumi ama ni ya kipentekote, au kuja katika chini ya kichwa cha utume uliopo sasa.

Hata kanisa ilivyo na misingi ***"mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii"*** **Efe 2:19-20,** hivyo ni, kujengwa juu ya ufunuo wa Yesu kristo ambao unaletwa na mitume na manabii, hivyo imani ya mtu binafsi inastahili kuwa imeimarishwa na kulindwa vizuri katika msingi wa kanuni za elimu ya Mungu. Wakati misingi imewekwa vyema, hivyo ni, kufundishwa na kutekelezwa, kanisa kwa pamoja laweza kukua hata ukomavu na utimilifu. Twahitaji kukubaliwa na Mungu kuenenda katika ukomavu (**Ebr 6:3)** na Mungu hatakubali kama misingi haijawekwa sawa.

<u>Hebu tuiangalie tena misingi ilioorodheshwa katika Ebr 6:1-2</u>.

KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI

Dhambi zote ni kazi zisizo na uhai lakini katika mazingira ya kitabu cha Waebrania, kazi zisizo na uhai haswa zinazotajwa ni kazi 'zisizo na uhai za dini' ya kiyahudi. Mwandishi anaendelea kulinganisha na kuonyesha jinsi ilivyo bora Agano jipya kuliko Agano la kale. Kila sadaka ya mwanadamu sasa imewakilishwa na sadaka ya Kristo; kwa hivyo sadaka ya mwanadamu ni kazi zisizo na uhai. Kwa hivyo sanasana taratibu zetu na mipangilio ya kanisa zinaweza kuwa ni kazi za dini zisizo na uhai, hakika zikizuia kukua kwetu kuufikia utimilifu, badala ya kulea na kusaidia kufatilisha kukua.

IMANI KWA MUNGU

Badala ya kazi zisizo na uhai kunakuwa na ***"Imani kwa Mungu"*** **–** kutoka kwa kazi kwenda kwa utiifu wa imani: kuamini katika, kubatizwa ndani ya, na kwa kujazwa na Roho wa Yesu Kristo, na kuzifanya kazi zilizowekwa wakfu **(Efe 2:10).** Mara kwa mara 'kanisa letu la mahali pamoja' linafanya kazi kulingana na taratibu za dini zilizoelezwa na tunafikiri tumefaulu wakati tunafanya kazi kulingana na taratibu hizo; na kila wakati neno la Mungu linapuuzwa. Ufunuo ni nadra na waumini hawakui mpaka ukomavu, kwa kazi zuri za roho, zikifanya kazi katika mwili wa kristo, zikileta uhai.

Mtihani mwepesi wa kujua kana kwamba sisi binafsi ama kwa pamoja tumewekwa msingi mwema ndani ya Krsto, na kukua ndani yake ndio mtihani wa kimaandiko ambao paul anaeleza: ***"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu?"*** **(2 Kor 13:5).** Wengine wanalazimishwa kwa hilo swali na wanatambua ya kwamba hawana uhusiano na Yesu Kristo. Na ni yeye peke yake anayeweza kutuokoa, anayeweza kutukomboa, anayeweza kutuponya. Ni Jina lake twapaswa kuliita. Hakuna jina lingine (**Mdo 4:12).**

MAFUNDISHO YA MABATIZO

Mabatizo (Kuoshwa) ni katika wingi. Ni nini 'Mafundisho ya mabatizo'? Wengine wasema inahusisha ubatizo katika Roho na hiyo ndio sababu iko katika wingi. Hata hivyo, ubatizo katika Roho ni kazi ya "***kuwekewa mikono***"na neno la kiyunani la 'mabatizo' ni 'kuoshwa', ikiangazia maji!

Agano Jipya linafundisha wazi kwamba kuna ubatizo MMOJA tu (**Efe.4:5**). Lakini kuna ubatizo tatu katika Agano Jipya unaotusaidia kuelewa ubatizo MMOJA. Ubatizo wa Yohana, Ubatizo wa Yesu na ubatizo wa waumini. Haya ndiyo mabatizo matatu ambayo tunastahili kufundishwa, ili huu msingi uwekwe sawasawa katika maisha yetu na ujuzi.

i. Ubatizo wa Yohana

- Ubatizo wa Yohana ulikuwa wa kuoshwa kwa **Maji.** ***"akawabatiza katika mto Yordani"*** **Mt 3:6**
- Ubatizo wa Yohana ulikuwa **wa toba.** ***"Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba"*** **Mdo 19:4** [ona pia **Mt 3:11; mk 1:4; Lk 3:3***]*.
- Ubatizo wa Yohana ulikuwa **Ubatizo wa ishara, ukimuelekeza Yule** aliyekua anakuja baadae, Masihi Yesu. "***Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya"*** **Lk 1:17,** [Ona pia **Lk 3:16; Mk 1:7-8; Mt 3:11; Yn 1:33**].
- Ubatizo wa Yohana ulikuwa **mapenzi ya Mungu** kwa watu. Mungu alilmtuma Yohana kutengeneza njia ya Masihi. **"*Lakini, mafarisayo na wana sheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye"*** **Lk 7:30**

ii. Ubatizo wa Yesu

- Ubatizo wa Yesu ulikuwa katika **<u>maji.</u>** ***"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini"*** **Mat 3:16.**
- Ubatizo wa Yesu ulikuwa ni ubatizo wa Masihi mwenyewe; **<u>kutimizwa kwa ishara:</u>** Yesu aliye Masihi alibaizwa. ***"Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe"*** **Mat 3:13**
- Ubatizo wa Yesu sio wa toba toka kwa dhambi, lakini ***"kutimiza haki yote"*** **aya 15**
- Wakati Yesu alibatizwa ***"na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake"*** **Mt 3:16.** Kuja kwa Roho na njia hii ni mpya kabisa. Mtu duniani anaweza kujazwa Roho wa Mungu.
- Wakati wa ubatizo wa Yesu, **sauti kutoka mbinguni, ikimpa uwana (Mt 3:17).** Ambacho Adamu alikuwa amepoteza ilikuwa sasa imerejeshwa katika Yesu na zaidi sana kwa sababu Roho wa Mungu alikuwa sasa akikaa na mwanadamu kikamilifu. Yesu hakuwa tu 'nafsi inayoishi' lakini roho ipatianayo uzima' **(1Kor 15:45).**
- Ubatizo wa ulikuwa **mapenzi ya Mungu kwa Yesu:** ***"kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote"*** **Mt 3:15**

iii. Ubatizo wa waamini - <u>Kutimizwa kwa ubatizo wa Yohana na ubatizo wa Yesu</u>.

- Ubatizo wa waamini ni **<u>kuwekwa ndani ya maji</u>. "*Yule toashi akasema, 'Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe"'*** **Mdo 8:36.** Tambua, neno la kiyunani 'ubatizo' inamaanisha 'kuingizwa ndani/kutumbukizwa ndani ya maji' sio kunyunyiziwa. Hapana ubatizo wa kunyunyiziwa ulionakiliwa katika Biblia.
- Ubatizo wa waamini ni wa **<u>kutubu na kuondolewa kwa dhambi, (</u>Mdo 2:38).**

- Waamini **<u>wanabatizwa katika Masihi, ishara inaonekana</u>. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo tuenende katika upya wa uzima"* Rum 6:4, *[*ona pia **Gal 3:27; 1 Kor 12:13***/***
- Waamini wanabatizwa **ndani ya JINA la Yesu Masihi** (Kristo). ***"Mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"* Mt 28:19;** hivyo ***"katika jina la Yesu Kristo"* Mdo 2:38; "*Wakabatizwa katika jina la Yesu Kristo"* Mdo19:5.**
- Waamini wanastahili **<u>kupokea Roho Mtakatifu</u>** kama matokeo ya ubatizo kwa "***ondoleo la dhambi"* Mdo 2:38. *"Wakati Paulo aliwawekea mkono [***baada ya ubatizo wa maji] ***Roho Mtakatifu akaja juu yao"* Mdo 19:6.**
- Ubatizo unaweza kuwa ni wakati wa **<u>kupokea neno la kiunabii</u>** likitangazwa katika maisha ya muamini, kama ilivyokuwa kwa Yesu na Paulo **(Mdo 19:15-18).**
- Ubatizo ni **mapenzi ya Mungu kwa kila muamini, [Mk 16:16; Mat 28:19].**

KUWEKEA MIKONO

Kimsingi kupokea Roho Mtakatifu – njia ya kawaida ya kupokea Roho Mtakatifu ni kwa kuwekea mikono. Wayahudi katika siku ya pentekote (**Mdo 2:4),** na wayahudi katika nyumba ya Kornelio (**Mdo 10:44-46),** walipokea nguvu na kumuagiwa na kujazwa na Roho Mtakatifu. Wale waamini elfu tatu siku ya pentekote wangepata kuekewa mikono juu yao (**Mdo 2:38; 41).** Waumini waliobatizwa samaria walipokea wakati mitume waliwawekea mikono: ***"Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakapokea Roho Mtakatifu" (*Mdo 8:17).** [Ona pia **Mdo 9:17** na **Mdo 19:6**]

Kuwekewa mikono pia ni kwa uponyaji na kutumwa na kusimikwa, kuachiliwa kwa karama na huduma.

KUFUFULIWA WAFU

Wakati tunabatizwa tunainuliwa pamoja naye katika maisha ya ufufuo. Kufufuliwa wafu ni uhakika tu kwa sababu Yesu alikufa na hakika akainuka katika wafu siku tatu baadaye, ***"Mzaliwa wa kwanza katika wafu***" (**kol 1:18**).

Kufufuka kwa Yesu ndio msingi wa uzima wa milele; kwa maana Alifufuka, twaweza kupokea uzima wa milele kama alivyo sasa ***"Roho yenye kuhuisha"* (Yn 5:25** na **1Kor 15:45).** Yesu alisema "***Naye kila aishie na kuniamini hatakufa kabisa hata milele" (*Yoh 11:26).** Kufufuka kwa Yesu kunaelekeza kwa maisha ndani yake katika maisha ya kila mwamini.

Maisha ya kufufuka yanastahili kuwa ndio mtindo wa maisha ya wakristo lakini pia ni lengo la kufikia. "***Ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake. Ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu"* (Flp 3:10- 11).**

HUKUMU YA MILELE

Inatangazwa katika injili "***Atakayemuamini asipotee bali awe na uzima wa milele***" (**Yn 3:16**).

Tunatawaliwa na umilele; lazima tuchague sasa, tutakayemtumikia. Hukumu ya milele inategemea vile unamuitikia Yesu.

'*Sema ombi la mwenye dhambi'* mtazamo wa uzima wa milele - '*sasa utaenda mbinguni'*- imedunisha msingi wa Biblia wa hukumu ya milele. Hukumu imetuzingira, na kila

siku, ni iwe tunaishi katika amani ndani ya ufalme au tunang'ang'ana katika ziwa la uutu. ***"Akatuhamisha na akatuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake***" (**Kol 1:13**).

"Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la mwana pekee wa Mungu" (**Yn 3:18*****).***

KUENENDA KATIKA UKOMAVU

Wakati kanuni za msingi zinafundishwa na kutekelezwa, hapo kanisa ***"linaweza kuenenda katika utimilifu"*** **(Ebr 6:1).** Mungu atatujalia (**Ebr 6:3).** Lengo la Mungu ni kanisa kamilifu ambalo limekua kikamilifu, mwili uliokomaa wa waamini wakifanya kazi katika upendo wa *agape* ndani ya mwili wa Kristo.

Watu kama hao watamfuata Mungu (**Efe.5:1).** Kutoka kwa watu kama hao, kazi ya Bwana itavuma kila mahali (**1The.1:8**). Watu kama hao ***"wamemgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli; na kumngojea Mwanawe kutoka mbinguni, ambaye alimfufua katika wafu, naye ni Yesu, mwenye kutuokoa na ghadhabu itakayokuja"*** **(1 The 1:9-10).**

KUISHI MAISHA YA UTIMILIFU

"*Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu [ukamilifu, ukomavu kamili, kutimiliza lengo la mwisho]. Na hayo tutafanya Mungu akitujalia"* Ebr 6:1a na 3.

Mara misingi inapowekwa, hebu tusonge mbele. Kuna picha nyingi za kanisa katika ukomavu, au kanisa likija katika utimilifu, au kanisa likifanya kazi katika njia ya ukomavu maagizo ya Maandiko – Yesu alisema ***"mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"* Mt 28:19.**

Kwa mfano, katika **Efe 4,** Paulo anaangazia picha ya ajabu ya kanisa likija katika ukomavu kupitia huduma iliyofaulu ya mitume, manabii, wahubiri, wachungaji na waalimu: kanisa ambalo linalokua ***"katika mambo yote ndani yake yeye aliye kichwa - Kristo"* aya 15.**

Katika **1 Wakorintho**, sura **12, 13 & 14**, Paulo anaonyesha vile kanisa komavu linahudumu karama katika upendo kwa kulijenga kanisa lote.

Katika **Wakolosai 3:1-4:6**, Paulo anatueleza tabia za mtu mpya, tukianzia na mawazo yetu na uguzo kwa Bwana, tukishughulikia kila eneo la dhambi kuu, tukishughulikia nia ya moyo kwa wengine, na kisha "***kuuvaa utu mpya" (aya 12),*** na hatimaye kutuelekeza juu ya jamii na uhusiano wa kazi.

Mtazamo wa maisha yaliyokomaa – Warumi 12:9-21

Katika **Warumi 12** aya **9 -12**, Paulo anatuelekeza jinsi ya kukaa kama wakristo. Maelekezo katika aya hizi yako wazi sana na inahitaji kuwajibika katika kila hali tunapo tafuta kuishi maisha ya Ukristo, **kuishi maisha matimilifu.**

1. ***"Pendo na lisiwe na unafiki"* aya 9:** upendo ni jina *agape* na inamaanisha 'hisia za upendo na rehema'. Ni aina ya upendo wa Mungu na ni upendo ambao tunapaswa kuwa nao kwa mmoja na mwingine; ni upendo uliokomaa.
   Yakobo 3:17 inatuambia kwamba hekima itokayo kwa Mungu haina unafiki. Mnafiki ni yule anayejifanya.

2. ***"Chukieni lililo ovu"* aya 9.** Kuchukia maana yake ni 'kuchukia kabisa, kutopenda sana'. Hii inajumuisha uovu unaokuja ndani ya nyumba yetu tunapowasha televisheni.

3. ***"mkiambatana na lililo njema"* aya 9** mme au mke wanaapaswa kushikamana katika ndoa. Tunatakiwa kuambatana na lililo njema kwa bidii hiyo.

4. ***"kwa pendo la undugu, mpendane ninyi kwa ninyi"* aya 10.** Katika agano la kale Mungu alijulikana kwa utu wema na rehema kwetu – yuko vile vile leo. Katika **2 Pet 1:2-11,** Petro anatuambia hatua za ukomavu - kuishi katika "rehema" (KJV). Upendo wa undugu ndio hatua ya mwisho kabla haujaanza kufanya kazi katika upendo wa kweli wa Kristo.

5. ***"kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu"* aya 10.** Paulo anatuambia katika **Wafilipi *"kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake*** na ***kila mtu aangalie mambo ya wengine"* (Flp 2:3-4).** Tunapaswa ***"kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa"* 1Kor 12:23.**

6. ***"kwa bidii, si walegevu"* aya 11.** Tunapaswa kuwa ***"na bidii [jitahidi] kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayarika, ukitumia kwa halali neno la kweli"* 2Tim 2:15.** Una uhusiano wa kujipatiana na neno la Mungu? ni chakula unacho hitaji kila siku? Waamini wanatakiwa kuwa na jitihada katika kazi za kawaida: "***ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula"* 2 The 3:10.** Twatakiwa kufanya kazi na mikono yetu "***tupate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji"* Efe 4:28.**

7. ***"mkiwa na juhudi katika Roho zenu"* aya 11.** Juhudi inazungumza juu ya kujipatiana. Wakati mwingine bidii yetu inaweza kuwa ni ya kuhuzunisha na ilete mabishano na kuvunjika moyo. Kujipatiana kwetu kunatakiwa kuwe juhudi katika moyo. Ni neno la Mungu likigawa kati ya moyo na nafsi (**Ebr 4:12**).

8. ***"mkimtumikia Bwana"* aya 11.** Paulo alisema ***"nimuabuduye kwa roho yangu katika injili ya Mwana wake"* Rum 1:9.** Kama wana ***"basi si afadhali sana kutii chini ya Baba wa roho zetu na kuishi?"* Ebr 12:9.** Maisha ya mkristo yanaanza na kuzaliwa upya na Roho wa Mungu akituwezesha kumpokeaYesu. Tunazaliwa mara ya pili ili tutumike.

9. ***"kwa tumaini, mkifurahia"* aya 12.** Wengi wanafanya makosa ya kutumaini mambo ya mda mfupi na wakati kile wanatumaini kisipofika, wanavunjika moyo. Tumaini la kweli ni la mambo ya kudumu, mambo yanayohusu ufalme wa Mungu na tumaini la kweli ***"halitahayarishi"* (Rum 5:5**). Kama tumaini letu limewekwa kwa neno la Mungu, ni, ***"kama nanga ya roho"* (Ebr 6:19).** Tunapaswa kushikilia ***"kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na furaha ya taraja letu mpaka mwisho"* Ebr 3:6.** Ni kushikilia huku kwa tumaini ambako kunapaimarisha pahali petu ndani ya nyumba ya Mungu **(Ebr 3:6).**

10. ***"Katika dhiki, mkisubiri"* aya 12.** Neno 'dhiki' inamaanisha kufinywa. Nafikiri sote tunajua kufinyiliwa na uzito wa maisha lakini pengine hatujatambua mambo kama hayo ndiyo dhiki ambayo Biblia inazungumzia. Mungu anatupa neema kupitia imani ndani ya Yesu Kristo ***"tufurahi katika dhiki pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo, na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"* Rum 5:3-5.** Tambua pahali pa tumaini na kile tumaini inaleta.

11. ***"katika kusali, mkidumu"* aya 12.** Maombi yanapaswa kuendelea na kama yule mjane aliyefuatilia (**Lk 18:1-8**), ni kwa yule anayefuatilia akijipatiana atakaye jibiwa na Mungu. Kuna kuhimizwa kwingi kuhusu maombi katika agano la kale na agano jipya. Je, maisha yako yanafuatwa na maombi ya kuendelea?

12. ***"kwa mahitaji ya watakatifu"* aya 13.** Kanisa la kwanza ***"waliuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja"* Mdo 2:45.** Kila mmoja wetu anapaswa alipwe kazi ili "***apate kitu cha kumgawia mhitaji"* Efe 4:28**

13 ***"inayotolewa ukarimu"* aya 13.** Tunapaswa kuw wakarimu, bila kusahau ***"kuwakaribisha wageni; kwa maana kwa kufanya hivyo wengine wamewakaribisha malaika bila kujua".*** Tunayaona hayo katika nyumbani kwetu na katika kituo chetu cha mafundisho, tukipata vyakula pamoja katika ushirika ni ya muhimu sana katika kujenga uhusiano katika mwili na kuwajulisha 'wageni' katika mafundisho ya kitume.

14 **(a)** ***"Wabariki wale wanaowatesa ninyi"*** **aya 14.** Yesu alisema, ***"heri ninyi watakapo washutumu na kuwaudhi"*** **Mt 5:11.**
(b) ***"Bariki na wala usilaani"*** **aya 14.** Yesu alisema ***"wabarikini wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi"*** **Lk 6:28.**

15 **(a)** ***"furahini pamoja nao wafurahio"*** **aya 15.** Wakati mshiriki wa mwili anatukuzwa ***"viungo vyote hufurahi pamoja nacho"*** **1 Kor 12:26.**
(b) **"*Lieni pamoja na waliao"*** **aya 15.** Wakati mshiriki wa mwili anaumia, ***"viungo vyote huumia nacho"*** **1 Kor 12:26.**

16 ***"Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi"*** **aya 16.** Tunapotembea katika ukomavu, ***"na tuwaze hayo… na tuenende katika lilo hilo"*** **Flp 3:15-16.** Kuna nia iliokomaa – nia ya moyo – ambayo twapaswa kuwa nayo. Tunapaswa kuwa na nia nzuri na yenye nidhamu sio kuwa kigeugeu.

17 ***"msinie yaliyo makuu"*** **aya 16.** Lakini njoo kwa Yesu ***"ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo"*** **Mt 11:29.** Tunapaswa kuangusha 'vitu vilivyoinuka' na ngome ambazo ziko kwa mawazo yetu na tunatakiwa ***"kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"*** **2 Kor 10:4-5**.

18 ***"mkubali kushughulishwa na mambo manyonge"*** **aya 16.** Yakobo anatuonya ya kwamba Mungu ***"aliwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme wake"*** **Yakobo 2:5**. Tunapaswa kushirikiana na wale ambao Mungu amechagua. ***"Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima"*** **1Kor 1:26-27.**

19 ***"Msiwe watu wa kujivunia akili"*** **aya 16.** Hekima hutoka mbinguni na haitegemei uwezo wetu, kusoma kwetu au kitu chetu chochote **(Yakobo 3:17).** Mungu atapatiana hekima kwa ukalimu kwa wale wanauliza kwa imani (**Yakobo 1:5-6).**

20 **"*msilipe mtu ovu kwa ovu"*** **aya 17.** Inasemekana kumhusu Yesu ***"alipotukanwa, hakurudisha matukano"*** **1Pet 2:23.**

21 ***"Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote"*** **aya 17.** Paulo anatuagiza kutafakari juu ya ***"mambo yoyote yaliyo ya kweli… yastaha… ya haki… safi… na yenye kupendeza… yoyote yenye sifa njema…"*** **Flp 4:8.**

22 ***"mkae katika amani na watu wote"*** **aya 18.** Mithali inasema ***"njia za mtu zikimpendeza BWANA, hata adui zake huwapatanisha naye"*** **Mithali 16:7.**

23 **(a)** ***"msijilipize kisasi"*** **aya 19.** Kwa nini? Kwa sababu uamuzi wenu unaweza kuwa sio sahihi na mnaweza kumtesa mtu asiye faa.

(b) ***"bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa, asema Bwana"*** **aya 19.** Mungu huhukumu kwa haki; anajua moyo wa kila mtu. Ghadhabu katika sehemu yetu ni hasira ikitafuta kisasi. Mungu yuasema, ***"muwe na hasila ila msitende dhambi"*** **Efe 4:26.** Mungu anatuita tuonyeshe rehema na kutoa msamaha, tukimpatiana ambaye ametudhuru katika haki ya Mungu – **yeye atalipisha.**

24 ***"Lakini, adui yako akiwa na jaa, mlishe; akiwa na kiu mnyweshe; maana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake"*** **aya 20.** Tabia kama hiyo ni kinyume cha mtu wa kawaida. Hatutaki kuwalisha adui zetu; hatutaki kumpa kinywaji! Lakini Mungu anasema tukiyatenda hayo, ukalimu wetu hakika utaleta hukumu ya Mungu kwa adui kama hatatubu.

25 ***"usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema"*** **aya 21.** Yesu ***"kwa njia ya mauti alimharibu yeye aliyekuwa nguvu za mauti yaani ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa*** **Ebr 2:14-15.** Kwa maana Yesu ameharibu nguvu za shetani (**1 Yn 3:8b**), sisi pia tunaweza kuushida uovu. Uhakika wa kweli ambao tunapaswa kutafuta ni: kama mtu akikuinukia katika njia ya ukali (uovu), Jibu kwa upole. ***"jawabu la upole hugeuza hasira"*** **Mithali 15:1.**
Yohana anasema ***"kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu"*** na ***"huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu – hiyo imani yetu"*** **1Yn 5:4.**

Sehemu hii ndogo kutoka Warumi ni 'sheria' nzuri ya maisha kwetu katika kuishi maisha ya ukristo. Hivi punde nimekuwa ni kisoma habari za Count Zinzendolf, ambaye aliyekuwa 'baba' wa jamii ya Herrnhut ya Mravians. Jamii hii, iliyokuwa imeundwa na wakristo waliokuwa wakimbizi kutoka mateso kule Mravia mapema katika karne ya 18 na ambao walikaa katika nchi ya Count, walikuwa wandugu walioungana, wakijipatiana kikamilifu katika kumtumikia Mungu na kufanya sehemu yao katika kutimiza tume. Mapema katika kukua kwao walikubaliana kuishi kwa 'sheria ya kitume'. Nijapo kuwa sijui mambo ya ndani ya sheria hii, ninafahamu kuwa ilikuwa ni jambo la kutimiza aliyoyasema Paulo katika **Wafilipi 3:16** ***"lakini, hapo tulipofika na tuenede katika lilo hilo".***

Tunaamini katika kikundi cha SHILOH ya kwamba Mungu ametuita tuwe watu kielelezo, tukiishi kulingana na mfano wa kiutume wa Paulo na watu alioitanishwa nao; tukiishi kulingana na mfano wa kiutume ya kanisa la kwanza katika kitabu cha matendo ya mitume, tunashangaa ya kwamba sehemu kubwa ya kanisa inaishi kulingana na muundo uliowekwa na watu kihistoria na sehemu kubwa ya muundo huo hauna uhusiano na neno la Mungu kwa hivyo haiwezi kuzaa matunda ambayo Yesu anatazamia. Tunawauliza kokote mlipo kumuomba Mungu awape maono ya kweli ya jamii ya kikristo na kuhakikisha kwamba unejenga kulingana na **muundo uliofunuliwa,** ambao umewekwa wazi kwetu katika neno la Mungu.

KANISA LINAPOOMBA

Fujo katika mataifa

Nilipo safiri na kuhudumu katika Liberia katika Africa magharibi na kuhudumu katika vituo tofauti tofauti Kenya mnamo Mei/Juni 2008, nilitambua kwamba licha ya matatizo ya kitaifa mabaya katika mataifa haya, kanisa halikuwa limejipatiana, au likitia bidii katika, maombi ya pamoja yakiongozwa na wahuduma wao. Liberia inaendelea kupokea afueni kutoka miaka 14 (1989-2003) ya vita hatari sana za kijamii ambayo imeacha taifa likiwa na mshtuko unaosubua, kwa mauaji mengi yasiyoelezeka, majeraha hatari na ubakaji wa watu wasio na hatia.

Kenya ilipitia kipindi cha miezi miwili na nusu ya kutikiswa kukubwa mapema 2008, na nilishuhudia baadhi ya matokeo ya uharibifu wa mali katika miji na vijiji katika maeneo ya mashambani katika magharibi mwa Kenya. Mnamo alhamisi 29 Mei 2008, nilihudumia kikundi cha watu waliokuwa wametorokea mauaji, mambo ya uharibifu, wizi na uharibifu wa nyumba zao [majengo ya kanisa na shule].

Ni katika mazingira haya ambapo mtume Paulo anaagiza kanisa kila mahali, wajipatiane katika maombi "***kwa watu wote, kwa ajili ya wafalme, na wote wenye mamlaka",*** linakua na umuhimu na la dharura na kushughulikiwa kwa haraka katika ufahamu wangu. Kama tukiomba katika utiifu wa neno la Mungu na kwa kukubaliana na neno la Mungu, tutapata kujua matokeo ya ahadi ya Mungu ya kibiblia: "***tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu"*** **(1Tim 2:1-2).**

Omba kulingana na neno

Katika **1Tim2:1-4** Paulo anahimiza kanisa, "***nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu, Hili ni nzuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu, ambaye hutaka wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli"***

Nimepata kujua kwa miaka mingi kwamba kanisa linapokusanyika na maombi ya pamoja yanafanywa kulingana na aya hizi, kanisa linaanza kusimama kwenye pengo na Kristo Yesu ambaye ni mpatanishi: "***kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu ni mmoja mwanadamu Yesu Kristo" aya 5.*** Wakati kanisa **linaomba kwa kukubaliana na neno la Mungu** hapo kanisa litapokea matokeo ya mwisho ya maombi: amani na utulivu. Maombi kama hayo ni kitendo chenye nguvu cha vita vya kiroho, kama kanisa ilivyopewa mamlaka na Mungu kufanya maombi kama hayo katika jina laYesu aliye Msihi.

Katika kutupa ombi la Bwana, Yesu ametuagiza kuhusu vipengele muhimu za maombi. Kuna kuachiliwa kwa ufalme wa Mungu; kuna ubabanuzi wa mapenzi ya Mungu. Wakati kanisa linasimama katika kukiri makubaliano ya maombi kulingana na mapenzi ya Mungu, hapo maombi ya kanisa yataimarishwa (kujibiwa) na mapenzi ya Mungu itafanywa duniani.

Maombi kwa watu wote – 1Tim 2:1

Paulo anatuhimiza katika **1Tim 2:1** kwamba ni '***ya muhimu' (ama kabla ya mambo yote) "kwamba dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote".***

Alitaja aina tatu ya, au njia tatu za, maombi ya watu wote na vilevile kunatakiwa kuwa na kufanywa shukrani.

- **Dua**

Dua ni nini? Kamusi inasema ni kusihi, au kuomba kwa njia ya unyenyekevu ukifanya maombi, anazungumzia kuhusu kusihi yenye kumaanisha na kumlilia Mungu kwa ajili ya watu fulani (au watu wote).

- **Sala**

Sala ni nini? Sala zinahusisha dua lakini kijumla maombi ni mawasiliano yetu na Mungu. Hii inamaanisha maombi ni mazungumzo na ni lazima tusikilize jawabu zake. **Flp 4:6** inatuambia ni kwa sala na dua ambapo ***"haja zenu na zijulikane na Mungu".*** Tunajua kwamba Mungu ametujibu kwa ushahidi wa ***"amani ya Mungu"*** **aya 7** ikija kwa nafsi yetu. Sala na dua zinapaswa kufanywa ***"katika Roho"*** **Efe 6:18.** Hii inamaanisha kuwa katika maisha yetu ya sala tunapaswa kutoka kwa upeo wa nafsi na kuingia katika upeo wa roho, ambapo Mungu anaweza kutuelekeza.

- **Maombezi**

Maombezi ni nini? Kufanya maombezi ni kwenda kwa niamba ya au kwenda katikati. Ni kusihi kwa niaba ya mwingine; inaweza kumaanisha kufanya kwenda katikati; inamaanisha kumwakilisha mwingine katika enzi ya neema.

- **Shukrani**

1 The 5:17-18 inatuambia ***"ombeni bila kukoma"*** na ***"shukrani kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu".*** **Efe 5:20** inatuambia ***"tumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote".*** Shukrani ni nia ya moyo wa mwaamini aliye jazwa na Roho na shukrani kwa Mungu ni nia ya kutupa usalama katika maombi yote.

- Maombi yapaswa kufanya kwa **WATU WOTE.**

Kuwaombea wote wenye mamlaka

Paulo kisha anaendelea kusema, ***"nataka wanaume wasali kila mahali, huku wakiinua mikono iliyo takatifu pasipo hasira wala mashaka; vivyo hivyo wanawake…"*** **1Tim 2:8-9a.** Katika makanisa mengi ombi ambalo tu linaombwa ni kumuuliza Mungu abariki ibada na kisha abariki sadaka na waliotoa. Kanisa lililokutanika linapaswa kuwa likiomba "***kwa watu wote, kwa wafalme, na wote walio katika mamlaka".*** Licha ya vita za kijamii kule Liberia na fujo za ghafla Kenya, kanisa linaweza kushikwa katika mtego wa kufikiria 'tunaenda kanisani kubarikiwa'; ila **kanisa linapaswa kuwa chemichemi ya baraka kwa taifa.**

Wakati Yesu alitakasa hekalu alitangaza ***"nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi"*** **Mt 21:13.** Alikuwa akinukuu kutoka **Isaya 56:7** ambapo Mungu alikuwa amesema ya kuwa sala katika nyumba yake yatakiwa iwe kwa **'mataifa yote'.** Katika mazingira mataifa ni '**watu wote'** ambao Paulo anatuambia tuombee.

Kuinua mikono mitakatifu

Tunaweza tu kuomba kwa dhati na kwa ufanisi ***"kwa kuinua mikono mitakatifu"*** **1Tim 2:8.** Tukiinua mikono yetu kwa Mungu na 'hasira, na mshaka' katika mioyo yetu tunakuwa wanafiki na mikono yetu sio mitakatifu.

- **Bila hasira**

Mwisho wa ombi la Bwana katika **Mt 6:9-13**, Yesu anahimiza mara ya pili umuhimu wa kuwasamehe wengine kama jambo linalohitajika kwa maombi yaliyojibiwa. Ghadhabu ni hasira ikitafuta kisasi. Biblia inasema, ***"muwe na hasira, ila msitende dhambi"*** **Efe 4:26.** Biblia inasema ***"wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitalipa, anena Bwana"*** **Rum 12:19.** Mungu anasema atafanya ghadhabu kwa maana ni Mungu tu anaweza kuamua kwa haki. Hata kama tuna sababu mzuri ya kukasirika na maadui zetu tunapaswa kumuomba Mungu neema ya kusamehe. Msamaha una nguvu kuliko ghadhabu. Ghadhabu inadhuru wengine na inamfunga mwenye kulipisa kisasi. Msamaha unakuweka huru na inaweka adui zako katika mkono wa Mungu. ***"Lakini adui yako akiwa na jaa, mlishe; akiwa na kiu mnyweshe; maana ufanyapo hivyo utampalia makaa ya moto kichwani pake"*** **Rum 12:20.**

- **Pasipo mashaka**

Paulo anasema pasipo kutilia shaka. Wakati maovu yanatendeka unaweza kushangaa 'Mungu yuko wapi?' Na mashaka yanaingia mioyoni mwetu. Yakobo anaonya tusipoomba kwa imani ***"hatutapokea kitu kwa Bwana"*** **Yakobo 1:6-7.**

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza" **Ebr 11:6.** Kabla ya kuomba kikamilifu tunahitaji ***"kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"*** **2Kor 10:5b.**

Kanisa limeitwa kusimama kwenye pengo katika maombi kwa ajili ya taifa. Kuyafanya haya kikamilifu tunapaswa kumsaidia kila mshiriki wa kanisa kukumbatia neema kuonyesha rehema na msamaha kwa wengine; na kuwa na kukiri kuzuri kwa imani katika ukuu wa Mungu na uwezo wake wa kuyajibu maombi yetu na kuokoa taifa letu.

Kwa hivyo ombeni

Kwa hivyo ninahimiza kanisa kila mahali wawe watiifu kwa maagizo ya Paulo katika **1Tim 2.** Kanisa linaweza kufanya tofauti katika taifa. Kanisa linapaswa kujua jinsi ya kuenenda ***"katika nyumba ya Mungu"*** **(1Tim 3:15).** Kila mara kanisa linakutanika ni vyema na ya kukubalika kwa Mungu kuomba kwa sababu ya taifa, kuombea watawala na wenye mamlaka.

Matokeo ya maombi kama hayo itakuwa ni amani katika taifa na nafasi kwa kanisa kuendelea na kazi ya huduma, tukiwaleta wote katika maarifa ya kweli.

Maombi kwa wafalme na wote wenye mamlaka – 1 Tim 2:2

Tunapaswa kuwaombea watu wote na kisha tuombee haswa wafalme - maraisi, mawaziri wakuu – na wote walioko kwenye mamlaka, hivyo ni, nafasi za ukuu katika jamii yetu na taifa.

Matokeo ya maombi kama hayo yatakuwa ***"utulivu na amani".*** Ni mataifa mangapi na ni miji mingapi ambao hawana baraka ya "***kuishi maisha yaliyo jaa na amani na utulivu katika utauwa wote na ustahivu"?*** Kanisa linaweza kusimama na kuuliza swali hili: ni kwa nini hakuna amani katika taifa letu? Katika mji wetu? Jawabu ni: kwa sababu kanisa halijapatiana nafasi ya kwanza kwa maombi kwa taifa, kwa watawala na wenye mamlaka.

Mapenzi ya Mungu ni mema – 1Tim 2: 3-4

Ni vyema "***hili ni nzuri, nalo lakubalika mbele za Mungu mwokozi wetu"*** ili tupate kuomba kwa bidii na kujipatiana kwa watu wote na serekali za taifa letu. Ni mapenzi ya Mungu sisi tupate kuishi "***maisha ya utulivu na ustahivu".***

Lengo la maombi yetu kwa watu wote, ikihusisha watawala, ni wokovu wao. Mungu ***"hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli".*** Mungu "***hapendi mtu ye yote***

***apotee, bali wote wafikilie toba"* (2 Pet 3:9).** Watu wataokolewa wakati watakuja katika ufahamu wa ukweli. Watasikia ukweli namna gani?

Kuna mpatanishi – 1 Tim 2:5

Ayubu alijua hitaji lake la mkombozi; alimhitaji mtu aende mbele za Mungu kwa niaba yake. Rafiki zake hawangemsaidia (**Ayubu 19:25).** Mara tu Kristo amekuja, Paulo anatangaza, ***"Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mtu Yesu".*** Ujumbe mkuu katika Agano Jipya ni kwamba "***Yesu ndiye Masihi" Mdo 5:42.*** Matokeo ya kifo cha Kristo ni ili ***"tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri"* (Ebr 4:16)** na kwa ujasiri tunaweza ***"kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu"* (Ebr 10:19).**

Alijipatiana kuwa ukombozi kwa wote – 1Tim 2:6

Dhamani ni gharama ya ukombozi. Picha hii inatoka kwenye soko na iliongea kuhusu kuununua uhuru wa mtumwa. Ukombozi kwa watu wote wapate kuokolewa ilikuwa ni damu ya Yesu: uhai wake. Alijitoa ili tuwekwe huru kutoka kwa utumwa na uharibifu wa dhambi na mauti.

Inaweza kuwa ni mtego kwa wakristo kuwa na kufurahia wokovu lakini kusahau ya kuwa Yesu aliutoa uhai wake kwa watu wote. Kanisa linalo endelea mara kwa mara linajiangalia na idara wanazojihusisha nayo. Ujumbe ambao ni lazima ishuhudiwe ni kwamba Yesu ***"alijitoa awe ukombozi kwa ajili ya wote".*** Ujumbe huo ni ***"utakaoshuhudiwa kwa majira yake"***

Hili ndilo jambo: ukweli wa Yesu ni nani, kwamba yeye ni Kristo (Masihi M**do 2:36**), kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu (Mungu akidhihirishwa katika mwili **1Tim 3:16**), kwamba yeye ndiye **njia tu** kwa Baba (**Yn 14:6**), na ya kwamba kupitia kifo chake watu wanaweza kuokolewa. Kwa hivyo ukweli wa kuwa Yesu ni nani na uhakika wa maandiko wa yale kifo chake kimefanya msalabani, "***utakaoshuhudiwa kwa majira yake".***

Kuchaguliwa kuwa mhuburi, mtume, mwalimu – 1 Tim 2:7

Matokeo yaliyo tarajiwa ya kanisa likitimiza wajibu wake kuomba kwa **"*watu wote, wafalme na wote wenye mamlaka"*** ni:

- Kwamba Mungu atawachagua wahubiri, mitume na waalimu ***"wa mataifa katika imani na kweli".***
- Huduma hizi zilizochaguliwa zinabeba wajibu wa kimsingi ***"kushuhudia"*** kuhusu Yesu aliye Masihi na gharama aliyolipa ili watu wapate kuokolewa.
- Huduma hizi zilizo chaguliwa zina beba wajibu wa kimsingi kuhubiri na kufundisha ***"maarifa ya ukweli"*** ili "***watu wote"*** wapate kuokoka.
- Kwa mapenzi ya Mungu kutendeka, kutakuwa na kuchaguliwa kwa wahubiri (hii inaweza kuhusisha manabii na wainjilisti kwa kuwa zote ni huduma za kuhubiri), mitume na walimu tena leo.

Utume ni kama alioupokea Paulo

Huduma hizi zilizochaguliwa zinapaswa kupeleka injili kwa mataifa. Mataifa ni wale ambao hawajaokoka. Wengi wa wanadamu hawajaokoka. Kuna hitaji kubwa ya maombi yaliyopangwa pamoja kwa watu wote ili Mungu ajibu na achague tena wahubiri, mitume na waalimu wa mfano wa Paulo.

Wito wa Paulo ulikuwa ***"alichukue jina langu (Yesu) mbele ya mataifa na wafalme na wana wa Isaraeli",*** Paulo alikuwa ***"Ateswe kwa ajili ya jina langu" Mdo 9:15-16.*** Katika siku hizi Mungu anatutuma kama wahubiri, mitume na waalimu na ametuamuru tuwashuhudie

mataifa, na pia kwa kondoo waliopotea wa Israeli ambao ni kanisa. Tunapaswa kuhubiri kwamba Yesu ndiye Kristo (Masihi – mfalme aliyekuja); kwamba Yesu ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

Kwa wafalme

Ujumbe wa kitume unaoendelea na unaopokelewa kwa mataifa mengi tayari umefika kwa viwango vya juu ya serekali za kijamii na ofisi za siasa katika mataifa hayo. Mimi binafsi nimesikia mhuduma wa serekali akiuliza mkutano wa nyumbani wangu na kikundi na akatuuliza kumuwekea mikono na kumuombea. Mmoja wa wana wetu, anayehubiri katika Afrika ya kati alipokea mke wa raisi na mhuduma wa serekali waliohudhuria mikutano yake. Kama matokeo raisi wa nchi ile aliuliza mtume mchanga katika taifa hilo aje afundishe katika kanisa lake la nyumbani.

Katika imani na kweli

Huduma hizi zilizochaguliwa ni ***"katika imani na kweli". "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"*** **Rum 10:17.** Imani hapa inazungumzia mafundisho, mafundisho ya kitume (**Mdo 2:42**) na ***"imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **(Yuda 3).** ***"Neno lako ndiyo kweli"*** **Yn 17:17.** Kuhubiri na kufundisha ukweli ni kuhubiri na kufundisha neno la Mungu ambalo linaleta imani kwa wanao sikiliza. Hii ni njia ya Mungu ambayo ***"Watu wote wapate kuokolewa".***

Kwa sababu ya kutofaulu kwa kanisa katika kuwafanya wanafunzi katika mataifa yote, wengi wametia shaka jia aliyopatiana Mungu ya kutimiza utume. Njia aliyopatiana Mungu kuwafikia mataifa. Shinda imekuwa ni kutotii kwa kanisa. Tumeshambaza udini (mafundisho ya dini) kuliko injili ***"katika imani na kweli".***

Kizazi kipya cha wahubiri, mitume na waalimu

Ni wakati wa kizazi kipya cha kimaandiko cha wahubiri, mitume na waalimu wainuliwe. Hawa hawatarudia kutangaza mafundisho ya dini; watahubiri na kufundisha neno la Mungu, neno la kweli, neno la injili, kama ilivyoandikwa. Sio wakati wa mashirika ya kanisa ya mji kukutanika na kusema mafundisho ya kitume ambayo iliandikwa na maaskofu na historia ya kanisa na sio mafundisho ya kitume.

Kanisa la mji linahitaji kupokea karama tano za huduma

Ni wakati wa mashirika ya kanisa ya mji kukutana tena kusikia mafundisho ya kitume katika imani na kweli. Hii inahitaji mitume wa kweli ambao wameitwa na kuchaguliwa na Yesu na ambao wanafahamu siri za ufalme na utukufu wa Mungu. Hii inahitaji waalimu ambao wamepokea na kufahamu mafundisho ya kitume. Hii inahitaji wahubiri ambao wanaweza kuhubiri injili ya ufalme wa Mungu, injili ya Yesu Kristo na sio mafundisho ya mwanadamu yalioghoshiwa.

Maombi na huduma ya neno

Wakati kanisa linaomba kulingana na mapenzi ya Mungu katika utiifu wa maandiko kama ilivyoandikwa, matokeo yatakuwa ya ajabu. Mungu amepatiana kanisani majukumu ya tume. Maombi na huduma ya neno ndio mambo mawili yenye umuhimu ya huduma ya mitume na kwa hivyo katika huduma zote (**Mdo 6:4)**. Hebu tujipatiane kwa maombi na tutaona kwamba Mungu atawainua mitume, wahubiri na waalimu ambao watalinena neno la Mungu. Amen!

HATUA ZA UTUKUFU

Kutii ndio jambo funguo

"Mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo" **Efe 5:21.** Watu wote wa Mungu wanapaswa kuwa wakitii mmoja na mwingine. **"*Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema"* (1 Pet 5:5).**

Kutii ndilo jambo la msingi, ikiwa ni nia ya roho pamoja na maamuzi ya mapenzi. Utiifu unawekwa pamoja na upole wa mawazo. Yesu alisema, **"*Kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo"*** na atatufundisha jinsi ya kuwa kama yeye (**Mt 11: 29).** Paulo alisema, "***kwa unyenyekevu wote na upole"*** **(Efe 4:2).** Unyenyekevu wote na upole ni mambo ya muhimu kwa kuweka ***"umoja wa Roho".*** Yakobo anasema kwamba hekima itokayo juu ni ***"ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu"*** **(Yakobo 3:17).** Utiifu kwa Mungu ndio funguo kwa ushindi juu ya shetani (**Yakobo 4:7).**

Inaonekana sisi sote Mungu atatuweka katika hali ambazo zinaonekana kuwa kinyume na 'mapenzi yake, yaliyo mema na makamilifu ya kukubalika' ili tujifundishe kutii. Hata katika kuwekwa kwetu kanisani au nyadhifa zetu za kazi Mungu anaweza kuwa kazini ndani yetu kwa kuwaweka watu wengine katika maisha yetu ili tujifundishe kutii. Utiifu sio tu kwa wale ambao ni vyepesi kuwatii – Utiifu ni nia ya moyo na mtu anaweza kujifundisha.

Utiifu kwanza ni kwa Mungu na hakika twastahili kumtii. Pili, utiifu ni kwa wale ***"wenye kuwaongoza"*** **(Ebr 13:17).** Tunaishi katika kizazi kisichonyenyekea na chenye kuasi na hata kanisani wengi wanakataana na uongozi. Tatu utiifu ni kwa mmoja na mwingine katika mwili wa Kristo.

Unyenyekevu funguo ya neema

Utiifu ni funguo ya kunyenyekea. Mtu mtiifu ni mtu mnyenyekevu na unyenyekevu ni funguo ya kupokea neema. **Yakobo 4:6** inasema, ***"Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu".*** Hii inathibitisha **1Pet 5:5b.** Petro aendelea kusema, ***"Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake"*** **(1Pet 5:6).** Kuinuliwa kwetu na Mungu ni kazi ya neema na neema inapokelewa kupitia imani. Imani ni karama ya Mungu ambayo inatambulika ndani ya maisha yetu wakati tunapata njaa ya kumgeukia Mungu; kwa njia ingine tunafanyisha imani kazi ambayo inatokana na unyenyekevu – hatuwezi kufanya kwa nguvu zetu.

Unyenyekevu ni kinyume cha kiburi. Mtu wa kiburi atakataliwa na Mungu na ataanguka. Mtu mnyenyekevu atasaidiwa na Mungu na atapata kibali [neema] katika kila hali, katika kila uhusiano. Hakuna sheria ya kuongoza unyenyekevu lakini kiburi kinaelekeza kwa maisha hoi. ***"Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza"*** **(Yakobo 4:10).**

"Kiburi cha mtu kitamshusha; Bali mwenye roho ya unyenyekevu ataheshimiwa" **(Mithali 29: 23).** Mungu anadumu na *yule* **"*aliyetubu na kunyenyekea",*** na ***"atazifufua roho za wanyenyekevu"*** **(Isaya 57:15).**

Neema fuguo ya huduma

"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo" **1Pet 4:10-11.** Huduma katika neno na utumishi zinawezekana tu kwa neema. Ni kwa ***"neema ya Mungu pamoja nami"*** inayofanya kazi ***"kwa utele"*** kupitia Paulo ambayo anakamilisha kazi ya Mungu **(1Kor 15:10).** Huduma inayofaulu ni kazi ya neema.

Paulo anasema kwamba alipokea ***"uwakili wa neema"*** kufanya ujulikane ufunuo wa siri **(Efe 3:2-4**). Paulo alisema ya kwamba ***"alifanyika mhuduma kulingana na karama ya neema ya Mungu"*** **(Efe 3:7),** na ya kwamba aliweza ***"kuwahubiri mataifa"*** kulingana na neema ambayo alikuwa amepewa kama mhuduma. Pia katika **Wakolosai** Paulo anaongea kuhusu uwakili wa neema aliyopewa ***"kulitimiza neno la Mungu"*** **(1:25).**

Wengi wetu wamepitia miaka ya mwondoko wa Karismatiki ambapo himizo ilikuwa juu ya nguvu na karama na hata kama nguvu na karama ni za neema, hatukutembea katika neema hiyo. Sasa kwamba roho wa uwana unaachiliwa kwa wingi katika mioyo yetu, tunaanza kutembea katika neema hiyo kubwa ambayo Mungu ameweka juu yetu bure katika wapendwa (**Efe 1:5-6).**

Huduma funguo ya siri

"Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni" **Mt 13:11,** lakini tunahitaji mwalimu kuzifunua siri. Hakika, tunahitaji mtume ama nabii ambaye amepewa ufunuo na Roho **(Efe 3:5).** Ni mapenzi ya Mungu ***"ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa"*** **Kol 1:27.** Maarifa ya siri inapaswa ***"kufunuliwa kwa watakatifu"*** **(aya 26).** Ni kupitia huduma ya neno ambapo maarifa ya siri inajulikana. Haya ni mafundisho ya hekima ya ndani (**1Kor 2:6-7**).

Wengi wanasoma Biblia katika kiwango cha wepesi na wengi wanahubiri neno kwa kiwango cha chini. Kwa sababu ya ukosefu wa mitume wa kweli na manabii ambao wanaweza fanya kujulisha ufunuo wa siri, kanisa kwa jumla imewachwa katika hali ya kutokomaa. Katika siku zetu Mungu anainua mitume wa kweli na manabii ambao wanaweza fanya siri ijulikane, na mara tena kanisa linafanyika la kitume kwa kuyapokea mafundisho ya mitume (**Mdo 2:42 & yuda 3**). Mara tu kanisa linafundishwa Elimu na kisha mafundisho yanapitishwa na wahuduma katika kila kiwango **(2 Tim 2:2**)

Siri funguo ya utukufu

Ni kupitia huduma ya neno kwa ambao sio watoto katika Kristo (**Ebr 5:12**) lakini kwa wale wamekomaa (**1Kor 2:6**) kwamba ***"bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** **(aya 7)** inajulikana. Paulo anasema ya kwamba ni hekima hii ambayo inafunua utukufu wa Mungu ndani yetu. Kwa Wakolosai alisema ya kwamba ni kwa kutimiza huduma ya neno ambapo siri inajulikana kwa watakatifu na hii ni ***"utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa: nao ni Kristi ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:25-27.**

Utukufu ni nini? Je tunaweza kuutambua? Tunaweza kuelewa? Kukua katika utukufu? Yesu ndiye udhihirisho au ufunuo wa utukufu wa Mungu: ***"Naye neno alifanyika mwili, akakaa***

kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" **Yn 1:14.** Utukufu ni 'neema na kweli' katika maisha ya mwanamume ama mwanamke. Utukufu wa Mungu unafunuliwa juu na kupitia Kristo Yesu – anaangaza na kufunua utukufu wa Mungu! (**2 Kor 4:6**). Utukufu wake unastahili kuonekana kwetu, ***"katika vyombo vya udogo"*** **(aya 7).**

Utukufu funguo ya Umoja

Mungu alimuuliza Yesu arejeshe ***"utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako"*** **(Yn 17:5).** Kisha Yesu akasema ***"alikuwa ametukuzwa ndani yao"*** **(aya 10),** wanafunzi wake, na kama matokeo ya utukufu ukifunuliwa katika wanafunzi, wengekuwa **MMOJA (aya 11).**

Kisha Yesu akawaombea ***"wale watakaoamini kwa sababu ya neno lao (mitume) wote wawe na umoja"*** **(aya 20-21).** Yesu amepatiana utukufu wake kwa wanafunzi wake ili kupitia wao waamini wapokee utukufu. ***"Utukufu ule ulionipa nimewapa wao, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo UMOJA"*** **aya 22.** Lengo la Mungu ni kwamba utukufu wake ufunuliwe kupitia wanafunzi wake ili ***"dunia hii nzima itakavyo jawa na utukufu wa BWANA"*** **(Hesabu 14:21).**

Umoja funguo ya kuwa wakamilifu

Matokeo ya utukufu ukipewa wanafunzi na kupitia hawa kwa waamini wote ilikuwa ili watakatifu wawe mmoja katika ufunuo wa Uungu wote. Kumbuka kwamba "***utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili"*** **(Kol 2:9),** na ***"Kristo ndani Yetu tumaini la Utukufu"*** **Kol 1:27,** na ***"mmetimilika katika yeye"*** **Kol 2:10.**

Wakati Yesu yuko ndani yetu na Baba yuko ndani ya Yesu [ambapo kila mara yupo], kisha ***"***[***wanafunzi na waamini] watakamilika katika umoja"*** **Yn 17:23.** Wakati utukufu wa Yesu Kristo aliye wa milele unafunuliwa [au kuonekana] na waamini kisha upendo wa ajabu wa Mungu utafunuliwa duniani kupitia waamini na ***"ulimwengu ujue ya kuwa Baba alituma Yesu"*** **aya 23.**

Utiifu ndio funguo ya unyenyekevu
Unyenyekevu funguo ya neema
Neema funguo ya huduma
Huduma funguo ya siri
Siri funguo ya utukufu
Utukufu funguo ya umoja
Umoja funguo ya kuwa wakamilifu

MAHALI PA MUNGU PA KUDUMU

"Msingi wake upo Juu ya milima mitakatifu.
BWANA [Yahweh] ayapenda malango ya Sayuni Kuliko maskani zote za Yakobo.
Umetajwa kwa mambo matukufu, Ee Mji wa Mungu!" **Zaburi 87:1-3**

Aya hii inapendekeza kwamba Yakobo, akiwawakilisha watu wa Mungu, ana zaidi ya kikao kimoja, lakini Mungu anawapenda watu wake wadumu na yeye katika Sayuni kuliko vyote. Ni wapi pengine watu wa Mungu watadumu ila Sayuni?

Maandiko yanasema ***"Yahweh ayapenda malango ya Sayuni".*** Malango yanawakilisha pahali pa kiingilio cha mji na mamlaka katika mji. Mji huu wa Sayuni ni mji wa mfalme mkuu. Katika asili ulijulikana kama mji wa Daudi, lakini Sayuni ni makao ya Mungu:

"Kwa kuwa BWANA ameichagua Sayuni, ameitamani akae ndani Yake. Hapo ndipo mahali pangu pa raha milele, hapo nitakaa kwa maana nimepatamani" **Zaburi 132:13-14.**

Makusudi ya mungu ni wazi: atadumu Sayuni. Kwa hivyo watu wa Mungu wanapaswa kuja Sayuni.

Umeufikilia mlima Sayuni

Agano jipya inadhibitisha kuwa kama waamini katika Yesu Kristo tumeufikilia mlima Sayuni: ***"bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni"*** **Ebr 12:22.**

Wengi wamefikilia ya kuwa mwandishi wa Waebrania anaeleza 'mbinguni', na tunatazamia kwenda mbinguni. Hata hivyo maandiko yako wazi: '**mmeufikilia** mlima Sayuni'.

Mlima sayuni unaelezwa kuwa sawa na **mji wa Mungu aliye hai** na mji wa Mungu kwa pamoja ni kanisa la Mungu aliye hai. Hakika kufahamu Sayuni ni sehemu ya siri kubwa ambayo Mungu anafunua siku hizi.

Kanisa duniani linatamani ufufuo na nyakati za kuburudishwa kuwatia nguvu katika imani wanapomngojea Yesu aje ila Mungu anatufunulia katika maandiko ya kuwa kanisa ulimwenguni tayari limeunganishwa na Mungu Mbinguni na ya kuwa tayari kanisa limekuja kudumu na Mungu na Mungu anatamani kudumu miongoni mwa watu wake.

Ni milima ipi iliyo misingi ya Mungu?

Kama misingi ya Mungu iko katika milima mitakatifu na Sayuni ndio mlima aliouchagua Mungu kuwa mahali pake pa kudumu milele na watu wake, milima hii ni ipi ambayo inajumuisha misingi ya Mungu?

Katika maandiko kuna milima michache ya muhimu kulingana na yale yaliotendekea huko, lakini katika kuufikilia Sayuni ipo milima miwili haswa ambayo inazungumzia ujuzi wa kimsingi kwa watu wa Mungu katika kuja kumfahamu na kuandaliwa kudumu na yeye katika Sayuni.

Milima hii miwili ni:

- Mlima Moria – mlima wa sadaka
- Mlima Horebu katika Sinai – mlima wa kujidhihirisha kwa Mungu na kupokea sheria.

Hebu tuitazame milima hii miwili na tufahamu misingi inayofaa katika ujuzi wetu wa kukomaa katika maisha Yetu ndani ya Kristo pamoja na Mungu.

MLIMA MORIA

Katika **mwanzo 22,** Mungu alimuagiza Ibrahimu ***"ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia"*** **aya 2.** Wakati Ibrahimu alimfunga Isaka na akachukua kisu kumuua mwanawe (**aya 9-10), *"malaika wa Yahweh akamuita kutoka mbinguni"*** na akamshauri Ibrahimu (**aya 11-12**); na kisha Ibrahimu akaona ***"kondoo mme katika kichaka"*** na akamtoa kondoo badala ya mwanawe (**aya 13**).

Jambo la muhimu kulitambua ni kwamba Ibrahimu **hakuona** BWANA lakini **aliisikia sauti yake tu. "*Basi imani, chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo"* Rum 10:17.** Hatua ya kwanza katika kuja kumjua Mungu ni kusikia sauti Yake (neno Lake) na kuamini – tunaokolewa kupitia imani (**Efe 2:8**)

Mamia ya miaka baadaye hekalu ya Sulemani ilijengwa juu ya mlima Moria na hapa ndipo pahali pale ***"Bwana alipomtokea Daudi babaye, alipotengeza mahali pale alipoagiza Daudi, katika kiwanja cha kupuria cha Arauna Myebusi"*** **2 Nya 3:1.** Mlima wa sadaka unaelekeza msalaba wa Yesu na sadaka yake iliyokamilika kwa sababu ya dhambi zetu. Ni katika mazingira ya mlima wa sadaka ambapo tunaokoka kwa njia ya imani, na tunaweza kuokolewa, kwa sababu Yesu alikufa kama Mwana kondoo wa Mungu "***Aichukuaye dhambi ya ulimwengu"*** **Yn 1:29.**

Sikukuu ya pasaka ina msingi katika sadaka ya Mwana kondoo na sikuu yake inaonyesha msalaba waYesu Kristo na imani inayookoa. Mahali pa sadaka ya damu kwa dhambi ilikuwa ni sahemu ya nje **katika hema ya Musa** na madhabahu hayo pia yanaongea juu ya msalaba wa Yesu Kristo, na birika ya maji inaongea juu ya ubatizo wa waamini na neno la Mungu likiwa na mahali katika maisha ya mwamini.

Mlima wa kwanza wa msingi unawakilisha ujuzi wa kuja katika wokovu: **toba na imani ikihusisha ubatizo wa maji kwa ajili ya wokovu** wa mtu. Hii imewakilishwa katika maandiko na mlima Moria.

Tambua tena kwamba Mungu hakumtokea Ibrahimu katika mlima huo lakini alisikia tu sauti kutoka mbinguni. Yeye na Isaka waliokolewa katika tukio hilo kwa imani – Ibrahimu alikuwa mtiifu kwa sauti hiyo.

Wengi kanisani leo wamepiga kambi (kudumu) katika mlima Moria, hivyo ni, wanaamini katika sadaka ya kupatanisha ya Yesu juu ya msalaba na hata wanabatizwa kwa maji lakini ujuzi wao wa Ukristo umezuiliwa katika msingi huo wa kwanza wa wokovu. Makanisa mengi wanajitakia kudumu katika mlima Moria, hata wakifikiria wamefika katika hatima yao katika Mungu.

MLIMA HOREBU KATIKA SINAI

Mlima wa pili wenye maana ya kimsingi, katika ufahamu wa kuimarishwa kwa makao ya Mungu na watu wake duniani, ni mlima Horebu.

Horebu ndipo kwanza Musa alikutana na Mungu katika kijiti kilichowaka moto (**Kutoka 3:1**). Kulikuwa na kudhihirishwa kwa malaika wa BWANA katika miale ya moto katikati ya kijiti **aya 2.** Ilikuwa ni Horebu katika jangwa ya Sinai ambapo Musa aliwaleta Waisraeli kutoka Misri **(Kum 1:6, 19; 4:10, 15** na kwingineko).

Ni yapi yalitokea Horebu?

Mungu alijidhihirisha kwa njia za kutisha na ***"ngurumo na umeme, na wingu zito juu ya mlima, na sauti ya baragumu iliyolia sana. Watu wote waliokua kituoni wakatetemeka"*** **Kut 19:16.**

Katika Horebu Mungu alipatiana sheria. Hii ilikuwa ni **Pentekosti** ya kwanza! na sikukuu ya Pentekosti ilikuwa ndio sikukuu ya pili katika mwaka iliyosherehekewa na Waisraeli mpaka Yesu alipokuja. Pentekote ilitimizwa na Roho Mtakatifu kuja na kuandika sheria katika mioyo ya waamini.

Ujuzi wa Pentekote unaonekana na kudhihirishwa na Mungu kupitia Roho katika maisha ya mwamini. Hakuna maono wazi ya Yesu Kristo katika utimilifu wake lakini kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu kumtumikia. Zipo ishara na maajabu, uponyaji na miujiza katika ujuzi wa kipentekote.

Ujuzi wa kimsingi wa pili pia umewakilishwa na sehemu ya pili ya hema ya Musa, hivyo ni, pahali patakatifu ambapo makuhani waliingia kumhudumia Mungu. Waamini ambao wamepokea Roho Mtakatifu wanaweza kumhudumia Mungu kupitia sifa na ibada.

Hatima

Hata hivyo, fikio ya Waisraeli walipotoka Misri haikuwa mlima Horebu. Lakini mlima Horebu palikuwa pahali palipoamriwa pa kukutana na Mungu kuwatayarisha na kuwaandaa kwa safari ya jangwa lakini hatima ilikuwa wakati wote kufika katika nchi.

Mlima wa msingi wa pili ni wa muhimu na wa maana katika kuwaandaa watu wa Mungu kuja katika pahali pa kudumu pa milele katika Mungu ambayo inawakilishwa na mlima Sayuni. Hata hivyo watu wa Mungu hawawezi kuweka kambi yao Horebu. Kanisa la wakati huu mamilioni wa waamini na maelfu ya makanisa wameweka kambi yao Horebu. Watu wa Mungu wamekusanyika katika ujuzi wa kipentekote – ishara, maajabu, udhihirisho (ndimi) na kimakosa kuamini kwamba wamefika katika utimilifu wa kile Mungu alicho nacho kwa watu wake.

Lakini **Mungu anakusudia kudumu Sayuni!** Mungu anawapenda watu wake wote mahali popote wanadumu lakini makusudi yake na kusudi lake lililoelezwa vyema ni kwa watu wake wadumu naye katika mlima Sayuni.

MLIMA SAYUNI

Sayuni mwanzo iliimarishwa na Daudi kama **kiti cha utawala wake (Enzi)** na ilikuwa ni Sayuni ambapo Daudi alilileta saduku la agano kwa hivyo **uwepo wa Mungu ulidumu Sayuni.**

i) Kuna visima Sayuni

Siri ya Daudi kuweza kushika ngome ya Sayuni ilikuwa kujua kwamba kulikuwa na **visima vilivyofichika.** Yoabu alipanda mpaka kwenye mfereji wa maji na akawashinda Wayebusi **(2 Sam. 5:8**). Kutoka wakati ambapo Daudi iliimarisha 'serekali ya Mungu' katika mlima Sayuni, Sayuni ilifanyika ishara ya enzi ya Mungu na ishara ya mahali pa mwisho na pa kudumu milele pamoja na watu wake.

ii) Mungu atayarisha Sayuni

Kuna wakati ambapo Mungu ***"utasimama, Na kuirehemu Sayuni, Kwa maana ndio wakati wa kuihurumia, Naam, majira yaliyoamriwa yamewadia"*** **Zab 102:13.**

"Kwa kuwa katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu watakuwako watu watakaookoka, kama Bwana alivyosema; na katika mabaki, hao awaitao BWANA" **Yoeli 2:32 (c.f. Isaya 37:31-32).**

iii) Serekali ya Mungu iko katika Sayuni

"*Neno la Yahweh kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako. Yahweh atainyosha toka Sayuni fimbo ya nguvu zako. Uwe na enzi kati ya adui zako"* **Zab 110: 1-2.**

Zaburi 110 inaiweka wazi ya kuwa Mungu hutawala kutoka mlima Sayuni kupitia Masihi Yesu. Anatekeleza hukumu kwa wafalme, mataifa na kwa viongozi wa serekali.

iv) Utukufu uko Sayuni

Mungu ameahidi ***"kuijenga Sayuni, atakapoonekana katika utukufu wake"*** katika Sayuni **(Zab 102:16).**

Utukufu utafunuliwa Sayuni. ***"Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, Yahweh ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa sitara"*** **Isaya 4:5**

v) Hukumu inatoka Sayuni

"Tena waokozi [wakombozi] watakwea juu ya mlima Sayuni ili kuuhukumu mlima wa Esau; na huo ufalme utakuwa ni mali ya YAHWEH" **Obadia aya 21.**

Wakati watakatifu wanakuja katika ukomavu, wakiisha kua katika ujuzi wa kimsingi wa wokovu na wa kuhudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu, watakuwa kama ***"waokozi/wakombozi"*** wakitoka Sayuni. Hukumu inaachiliwa duniani kupitia watakatifu.

Ni kuhubiri na kufundisha kwa neno la Mungu kupitia huduma ambazo Kristo ameweka kanisani ambapo kanisa linakuja katika ukomavu. Mwishowe ni neno lililokomaa likitoka katika kanisa lote ambalo linaleta hukumu juu ya mamlaka na nguvu ambayo kwa wakati huu zinatawala mataifa kupitia watu wasio halali wakitoa mamlaka nje ya Kristo **(Efe 3:8-10).**

Hatima yetu ni Sayuni

Maandiko yana mengi ya kusema kuhusu Sayuni. Hatima yetu ***"huonekana Sayuni kila mmoja mbele za Mungu"*** **Zab 84:7.** Wale watakaokuja Sayuni ni wale ***"njia ziendazo Sayuni zimo moyoni mwake"*** **aya 5.** Safari hii inazungumzia watu wa Mungu wakija Yerusalemu kusherehekea sikukuu za mabanda. Sikukuu zote zilikuwa zikubukwe kila mwaka lakini sikukuu mbili za kwanza za pasaka na majuma na (Pentekote) mwanzo zilikuwa zimefanyika nje ya nchi. **Sikukuu za mabanda** zingefanyika tu katika nchi ya urithi katika mwisho wa safari au safari kutoka Misri mpaka kwa Nchi.

Sikukuu ya mabanda ilifanyika kuwa sikukuu iliyo ya muhimu zaidi na imeunganishwa kikamilifu katika kufahamu Sayuni – makao ya Mungu ya kudumu pamoja na watu wake. Sikukuu ya mabanda ni mfano wa Mungu akidumu na watu wake duniani.

Patakatifu pa patakatifu, sehemu ya tatu na ya mwisho katika hema ya Musa, ilikuwa ndipo uwepo wa utukufu wa Mungu ulidumu. Utukufu wake ulijulikana kama ***shekinah,*** na utukufu wake uling'aa kutoka Saduku la Agano.

Katika historia ya kanisa na tabia, sikukuu za mabanda zimesahaulika na kupuuzwa na badala yake zikawekwa sikukuu za Krismas ambazo zinamuabudu mtoto Yesu na kupuuza Mfalme ambaye anatawala na kutamalaki kutoka Sayuni. Uhakika wa kutimizwa kwa hema ya Musa ikipatikana katika kanisa la Yesu Kristo umechukuliwa na ukristo wa dini. Utukufu wa Sayuni umechukuliwa na utukufu wa kirumi wa papa, na wakataaji wa kiruteli, kwa utukufu wa kanisa ya uingereza na kiongozi wake wa kifalme, na mafundisho ya wa prebestelian na wengine. Washiriki wa makanisa hayo na ulimwengu wa wakristo kwa jumla wanaangalia uzuri wa dunia na ufanisi kuliko kutii kwa neno la Mungu na kwa unyenyekevu na kwa ujasiri kufanya safari kwenda Sayuni, wakienda safari ya utakaso katika ukomavu katika Kristo.

Ni wakati wa kanisa kuja Sayuni; kuja katika kutimizwa kwa sikukuu ya mabanda; kuja katika ujuzi wa utukufu wa Mungu. Haya ndiyo Paulo anazungumzia katika **Kol 1:26-28** wakati anaongea juu ya utajiri wa utukufu wa Mungu ukifunuliwa katika watakatifu. Ni ***"utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa: nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu".*** Kwa hivyo ni wakati wa neno la Mungu kuhubiriwa tena; ni wakati wa neno la Mungu kufundishwa, aya kwa aya, misingi ikiwekwa na kuonya kila mtu kwamba ukomavu katika Kristo ndio lengo (**Kol 1:28**).

Mungu aliongea katika Mlima Moria

Kila maisha ya mkristo inapaswa kuwa imeimarishwa vyema katika misingi iliyofundishwa vyema katika biblia kuhusu, kuzitubia kazi zisizo na uhai na imani kwa Mungu kupitia Yesu kristo. Hii inahusisha ubatizo wa kibiblia, sio kuwanyunyizia watoto katika imani ya wazazi wao katika sherehe ya idara, lakini ni katika msingi wa mtu binafsi kuzaliwa tena na Roho wa Mungu kuamini katika na kuwa na ujuzi wa kumjua Yesu Kristo.

Mungu alidhihirisha uwepo Wake katika Mlima Horebu

Kila mkristo anahitaji kujua kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu; kujua nguvu za Mungu za kuwaponya wagonjwa; kujua mamlaka ya jina laYesu kutoa mapepo; kuweza kuabudu na kuhudumu kwa Mungu kupitia sifa na sala na maombezi.

Lakini Mungu hudumu na watu wake katika Mlima Sayuni

Mungu anawaita watu wake nyumbani. Mungu aliongea katika mlima Moria, na imani ya Ibrahimu ikaonekana.

Mungu alidhihirisha uwepo wake katika ishara na maajabu na akapatiana sheria ikiwa imeandikwa katika mawe kwa watu wa Mungu katika Mlima Horebu (Sinai).

Lakini Mungu hakukaa katika Mlima Moria. Mungu hakukaa katika mlima Horebu. Mungu alitangaza kupitia Daudi kwamba atadumu Sayuni. Alimuelekeza Daudi kuteka mlima Sayuni katika asili na kuimarisha enzi ya Daudi huko. Kupitia Zaburi na kupitia manabii wa nyuma, Mungu alianza kuongea kuhusu Sayuni kama pahali pake pa milele pa kudumu. Aliongea mambo mengi kuhusu Sayuni. Tumetamatisha tu kwa baadhi ya mambo katika fundisho hili.

Agano jipya inatangaza ***"Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa Mbinguni"*** **Ebr 12:22.** Tumefik! Kila kitu ambacho Mungu anakusudia kwa watu wake kinapatikana sasa kwetu. Tunapaswa kuja! Tunapaswa kuwa watu wanaosafiri. Kanisa halijawasili lakini kanisa linatakiwa kuwa watu wanaosafari. Kufaulu kwa dini yetu ama

ushirika wetu wa kanisa la pahali pamoja sio lengo lakini kule kukumbatia na kuingia katika kusudi la Mungu ndilo lengo.

"Njoni, twende juu mlimani kwa YAHWEH, na nyumbani kwa Mungu wa Yakobo; naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake; kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la YAHWEH litatoka Yerusalemu"
Mika 4:2

KANISA! UFALME!

Ufalme wa Mungu ni pahali ambapo Mungu anatiiwa kikamilifu. Kutii huko ni kwa njia ya imani. Mungu hatiiwi katika asiri kwa kuwa asiri (viumbe) viko chini ya laana (**Rum 8:20-21).** Mungu hatiiwi na nguvu za mapepo [tawala na nguvu na mengineo] kwa maana yanadumu katika uasi wote kwa ufalme wa Mungu.

Ufalme wa Mungu ni udhihirisho wa haki ya Mungu (Rum 14:17). Haki ya Mungu inawekwa ndani ya mwamini kwa njia ya imani, hata kama ilivyokuwa na Ibrahimu **(Rum 4:5-25).** Tunaweza tu kuwa wenye haki kwa njia ya imani katika Yesu Mwana wa Mungu na kwa hivyo ufalme wa Mungu unaweza tu kudhihirishwa kupitia watakatifu, waamini wa kweli, washiriki wa mwili wa Kristo.

Yesu ndiye Kristo, ambayo ni tafsiri ya masihi. Masihi ni aliyepakwa, hivyo ni, mfalme aliyepakwa na kuhani aliyepakwa, ambao ni umoja na mtu mmoja. Kuna upungufu wa ufahamu wa Kristo: Kristo ni nani? Yeye ni mwana wa nani? Kristo/Umasihi wake unamaanisha nini?

Paulo anatwambia katika **Efe 3:8**, ya kuwa alipewa neema haswa kuhubiri **mataifa utajiri wa Kristo usiopimika**. Kwa nini tu kwa watu wa Mataifa? Kwa nini sio kwa Wayahudi vile vile? Utume wa Paulo ulikuwa **"*alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli"* Mdo 9:15.**

Wana wa Israeli walikuwa na historia na ufahamu wa Kimaandiko wa Masihi na kutarajia kuja kwake. Watu wa mataifa hata leo hawana ufahamu kama huo au matarajio na matokeo yake, tumehubiri mwokozi peke yake, pasina kufahamu Yesu ndiye mfalme katika mwili na Mfalme sasa anatawala kutoka enzi ya Daudi juu.

Yesu ndiye Masihi

Kama Masihi, Yesu ndiye Mfalme aliyepakwa. Wakati Yesu alifunuliwa kama Mwana wa Mungu hapa duniani, alikuwa ni udhihirisho wa Mfalme aliyepakwa, ambaye alikuwa ametabiriwa kama **"SHILOH",** mtawala mkuu atakayekuja kutoka Yuda (**Mwa 49:10).** Alikuwa mwana mkuu wa Daudi **(2Sam 7:12-14a).** Ndiye aliyekuwa ayatawale mataifa **(Zab 2 &110).** Yesu ndiye MFALME! Hakuna ufalme bila Yesu.

Yesu aliwaambia Mafarisayo ***"ufalme wa Mungu umo ndani yenu"* (Lk 17:21).** Mafarisayo walikuwa katika ufalme? La! Walitaka kumuua mfalme ambaye alikuwa miongoni mwao. Ambapo mfalme yuko pana ufalme.

Ufalme wa Mungu ni udhihirisho wa haki ya Mungu, amani, furaha; **ufalme wa Mungu uko ndani ya Roho Mtakatifu (Rum 14:17).** Yesu alisema ***"ufalme wangu si wa ulimwengu huu"* (Yn 18:36).** Ufalme wa Mungu ni ufalme wa Kiroho! Hapana mapepo katika ufalme wa Mungu. Wakati mapepo yanakemewa, Yesu alisema ufalme umefika **(Mt 12:28)**

Mahali tu ambapo ufalme wa Mungu unaonekana ni miongoni mwa watu wa Mungu ambao kwa utiifu wanamyenyekea! Mwili ambao tu unaweza kudhihirisha ufalme wa Mungu ni kanisa, hivyo ni, kanisa la kweli: viungo ambavyo vimeunganishwa na Kichwa, wakiwa wamewekwa katika mwili na Roho katika ubatizo! **(1Kor 12:12-13, 18).**

Kabla ya ubatizo ambao unatuweka katika mwili, ni lazima **tuzaliwe mara ya pili [kutoka juu] kwa Roho wa Mungu ili kuingia katika ufalme wa Mungu.** Ubatizo hautuwezeshi kuingia katika ufalme. Tunaingia katika ufalme kupitia kuzaliwa upya (**Yn 3:5-6**). Hata hatuwezi kuuona ufalme mapaka tuzaliwe mara ya pili (**Yn 3:3**). Mara tu tunapozaliwa mara ya pili, hivyo ni, kumpokea Yesu ndani ya mioyo yetu kwa imani, tukijua kwamba dhambi zetu zimesamehewa (**Yn 1:12-13**), kisha tunabatizwa katika Kristo, Masihi, Mfalme. Kanisa ni mwili wa Kristo; mwili wa Mfalme.

Kanisa ni nini?

Kanisa ni *ecclesia.* Hili ni neno la Kiyunani linalo tumiwa na Roho Mtakatifau la kanisa. Wengi wanasema kwa kifupi inamaanisha *wale walioitwa.* Haya ni kweli, lakini kiini cha neno hili ni nini? Neno hili linatoka katika tamaduni za kale za Kiyunani na haswa katika mji wa serekali ya Athene. Ilikuwa ni kusanyiko lililojulikana la wenyeji [wanaume wote wenye zaidi ya miaka 30]. Katika Athene *ecclesia* ulikuwa ni mwili wa wenyeji waliojukumika kuwachagua mahakimu na kuwa na neno la mwisho katika kupitisha sheria na katika vita na amani. *Ecclesia* waliochaguliwa katika kila mwaka, baraza la wazee walio husika katika serekali ya mji.

Wakati Yesu alisema ***"Nitalijenga kanisa langu"* Mt 16:18,** alikuwa akisema nini? Alimwambia Petro kwamba kwa kuwa petro alikuwa amepewa ufunuo wa Yesu kuwa **Kristo (Masihi)** na **Mwana wa Mungu [Mungu aliyefunuliwa katika Mwili],** sasa angesonga mbele na kulijenga *ecclesia* yake. *Ecclesia* ingekuwa na mamlaka kwamba milango ya kuzimu (mamlaka ya mwovu) haingeweza kushinda kanisa (mwili unaoongoza) ambao alikuwa akijenga.

Funguo za ufalme

Kisha Yesu akamwambia Petro ***"nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni" aya 19.*** Mamlaka ya kanisa yanaelezwa kama **Funguo za ufalme,** nguvu za kufunga na kufungua na mamlaka ya mbinguni [mamlaka ya mfalme].

Kwa sababu ya tamaduni, kuna mawazo mengi tofauti na mitazamo kuhusu kanisa. Kwa sababu ya mitazamo hiyo wengi leo wanaongea kuhusu ufalme, hivyo ni, kufahamu mamlaka ya Mungu duniani, kama ni kitu tofauti na kanisa. Tunaamua na kulitupilia kanisa katika msingi wa ujuzi wetu na mifano mingine ya idara za wanadamu zinazoongoza kanisa badala ya kufahamu kwamba:

Kanisa ni mwili uliochaguliwa na mfalme Yesu kutawala duniani kama chombo na mfano na udhihirisho wa ufalme wake, ufalme wa Mungu.

Mtu Yesu aliwakilisha ufalme wa Mungu kwa kuwa yeye alikuwa mtiifu kikamilifu hapa ulimwenguni. Mwili wa Yesu Kristo utawakilisha ufalme tunapokuwa watiifu kikamilifu. Katika **2Kor 10:3-6**, Paulo anatuambia jinsi ya kutembea katika ujuzi wa mamlaka ya utawala (kiroho) ambao unadhihirika kupitia nguvu za Mungu kuangusha ngome, tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka. Tunapaswa kuteka nyara kila fikira [kila kitu au upinzani wa mawazo] ipate kumtii Kristo. Matokeo yatakuwa yapi? wakati kutii kwetu kunakamilishwa, tutakuwa tayari kupatiliza maasi yote.

Yesu alisema ***"nitalijenga kanisa langu".*** Watu walichukulia kutoka kwa Yesu na kujenga kanisa kulingana na mawazo yao. Yesu hakusema 'nitajenga ufalme wangu'. Katika

siku za hivi punde wengi wametambua kwamba Yesu analijenga kanisa lake, na hivyo ni vyema; lakini sasa tunasema tunapaswa kuendelea kujenga au kupanua ufalme. Pia maelezo haya ya tunayopaswa kufanya ni ubatili na ina uhitaji kujenga kanisa kwa sababu tusipojizuia tutajenga kitu chetu.

Ufalme wa Mungu unaonekana katika himaya ya Kiroho:

- **Ni ufalme wa Mungu wa milele**
- **Ni utawala wa Mungu**
- **Hauwezi kujengwa**
- **Hauwezi kupanuliwa na sisi**
- **Lakini inapaswa kuhubiriwa na sisi**
- **Na utadhihirika kupitia sisi tunapokuja katika utiifu uliokomaa**

Mitume na manabii

Mitume na manabii sio msingi wa ufalme; hao ni msingi wa kanisa (**Efe 2:20**). Kazi ya huduma sio kujenga ufalme lakini ni ***"kujenga/ kuwakamilisha watakatifu, kuujenga mwili wa Kristo, kufanya kazi ya huduma mpaka"*** kanisa linakuja katika ukomavu (**Efe 4:11-13**), ukifunua kikamilifu utawala wa Mungu ulimwenguni.

Mitume na manabii wanapaswa kuzijuza siri ya kanisa; kwanza, kwamba mataifa ni mwili moja ndani ya Kristo pamoja na Wayahudi, na pili, kwamba ushirika wa siri unapojulikana, ***"hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"*** **(Efe 3:5-10).** Hii itaelekeza katika utiifu kamili wa "***vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi"*** kwa ubwana wa Yesu Kristo **(Flp 2:9-11).**

Ufalme unafunuliwa kanisani

Inaonekana kwamba wengi wanafikia kushika wazo la ufalme na bila shaka ufalme ni fundisho la injili, lakini katika kuyatenda hayo, kuna mambo mengi yasio sawasishwa yanayo hubiriwa na kanisa halieleweki.

- **Ufalme wa Mungu ndio urithi wa kanisa hapa duniani.**
- **Kanisa linapaswa kuwa serekali tawala ya ufalme wa Mungu.**
- **Mfalme, Yesu, atatawala, kuziweka sheria na sheria zake zitekelezwe kupitia *ecclesia* wake, kanisa.**
- **Kanisa ndio mabalozi wa Kristo!**
- **Washiriki wa kanisa wamechaguliwa kama wahuduma wa upatanisho kwa niaba ya Mungu ndani ya Kristo!**
- **Kanisa ni mwili wake ambaye ni mfalme na mfalme yuko ndani yetu!**

Kanisa lote ni *ecclesia*

Ni ya kupendeza kutambua kwamba katika baraza la kanisa la **Mdo 15**, kwamba mitume na wazee ***"wakakusanyika wapate kulifikiri neno hilo".*** Baraza liliamriwa na Roho Mtakatifu akimuongoza yakobo kushiriki kutoka **Amosi** na kupatiana ufahamu wa yale Mungu alikuwa akitenda. Baraza kisha wakahusisha kanisa lote katika maamuzi yao na ***"ikawapendeza… kanisa lote"*** **Mdo 15:22.** Walaka, ulioandikwa, uliandikwa na ***"mitume, wazee na wandugu"*** na uliandikiwa ***"wandugu walio wa mataifa" aya 23.*** Huu ni mfano wa ajabu wa *ecclesia* ikifanya kazi. Wenyeji wa ufalme wa Mungu (mbinguni) (**Flp 3:20**) wakifanyisha kazi jukumu

walilopewa kama walioitwa kutoka kwa miundo ya dunia kutawala katika ufalme wa Mungu ulimwenguni.

Ufalme na kanisa haziwezi kutenganishwa

Kinabii, **Isaya 2 na Mika 4** zinaongea kuhusu ufame (mlima) na kanisa, (nyumba ya BWANA) ukiwa ***"Utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea vikundi vikundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni twende juu mlimani, kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo".*** Mlima unaongea kuhusu kuimarishwa kwa ufalme wa Mungu ulimwenguni - umefanyika ufalme juu ya falme zingine zote, na kilele cha ufalme ni nyumba ya Mungu, ***"iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli"*** **1Tim 3:15.**

Kanisa ndio *ecclesia* ya ufalme wa Mungu.

Neno ambalo mataifa watapokea halikuji kutoka kwa ufalme; linakuja kutoka kwa kanisa. Kanisa kikamilifu lina umuhimu katika kuleta ufame kwa kuihubiri injili na kwa kulifundisha neno la Mungu, wakifanya sheria zake zijulikane. Matokeo ya *ecclesia* ya Mungu kuimarishwa kama mwili wa Kristo unaotawala ulimwenguni, kikamilifu ukihubiri na kuonyesha na kudhihirisha ufalme wa Mungu, ni kwamba mataifa watakoma kutoka kwa vita. Umeshawahi kufikiri kitakacho jiri wakati mataifa wataacha kutumia mabilioni ya pesa katika silaha na badala kujenga manyumba na kuleta afya na huduma za elimu kwa watu wote wa duniani. ***"Bali wataketi kila mtu chini ya mzabibu wake, na chini ya mtini wake, wala hapana mtu atakaye watia hofu; kwa kuwa kinywa cha BWANA wa majeshi kimesema hivi"*** **Mika 4:4.**

Kwa wakati huu *ecclesia* inaonekana mijini; itaishi katika mikoa; na itaishi katika nyumba za wandugu. Kanisa linapokuwa katika ukamilifu, ufalme wa Mungu utadhihirika kupitia kanisa mjini; kupitia kanisa la mjini, la mikoa; na katika kila eneo la pahali pamoja kupitia nyumba za watakatifu. Kusundi la Mungu la milele litatimizwa katika udhihirisho. Kusudi lake la milele tayari limetimizwa kupitia kuja kwa Yesu Kristo **(Efe 3:11, 2Tim 1:10).**

MITUME - WAJENZI WAKUU

Mtume ni nani?

Kuelewa 'mtume ni nani', tunapaswa kwanza kuelewa ama 'kutafakari' mtume, Yesu Kristo. **Ebr 3:1** inasema ***"kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu".*** Kama mtume, Yesu anaijenga nyumba ya Mungu, ***"ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho"*** **aya 6.**

Kwa wazi neno la Kiyunani *apostolos* linamaanisha 'aliye tumwa'. Yesu ndiye 'mtume' wa Mungu. Mtume anatumwa na mtu. Wale thenashara walitumwa na Yesu **(Yn 17:18**). Tunahitaji kufahamu kwamba neno 'kutumwa' katika **Yn 17:18** na katika baadhi ya aya zingine, ni neno la Kiyunani, *apostello,* ambalo linamaanisha kutuma, kutuma kama mjube au kuweka huru.

Mtume anatumwa na mtu na anatakiwa amwakilishe aliyemtuma. Yesu alitumwa na Baba na akamwakilisha Baba, hivyo ni, alifanya Baba ajulikane na watu. Ye yote aliyempokea Yesu alimpokea Baba (**Yn 14:9-10a**). Katika **Mt 10:40** Yesu aliwaambia mitume wakati kwanza alipokuwa akiwatuma, ***"awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenituma".***

Mitume katika Agano jipya

Hakika mtu anapoanza kuwatafuta mitume katika agano jipya, tunaona kwamba wananenwa kila mahali. Ni ya kushangaza sana kwamba kanisani ambalo sisi nisehemu yake, tunasikia tu kuhusu wachungaji. Hatusikii kuhusu mitume; tunaambiwa kwamba hakuna mitume leo; lakini tunadhania kwamba kuna wachungaji leo. Ni kwa mamlaka gani ambayo tunatumia kufanya maamuzi hayo?

Katika agano jipya, mitume wametajwa mara nyingi na watu 26 wanaitwa mitume, na inaonekana wengine wanatajwa. Hakuna pahali ambapo panatajwa wachungaji moja kwa moja ila katika **Efe 4:11** ***"naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu".*** Hakuna mtu mmoja ambaye anitwa mchungaji katika Agano jipya.

Ni kwa mamlaka gani unayosema kwamba wewe ni mchungaji? Kwa wengi ni kwa msingi wa dini au tabia za mwanadamu; sio kwa utauwa wa kiungu, na ilahali huduma zote katika kanisa la agano jipya ni kwa utauwa wa kiungu. ***"Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha"*** **1Kor 12:28.**

Mitume wanatajwa kwa jina

Wale mitume kumi na wawili wa mwana kondoo, Mathiya akichukua nafasi ya Yuda. Wale thenashara katika **Mathayo 10:2-4**; Mathia katika **Mdo 1:26.**

Mitume wengine waliopatianwa na Kristo katika kupaa kwake **Efe 4:11**
Paulo na Barnaba katika **Mdo 13:2, 14:14;**
Androniko na Yunia [na mitume wengine waliotajwa] katika **Rum 16:7**;
Apolo kwa kuhesabiwa katika **1Kor 1:12 na 4:**6; Apolo anatajwa na Paulo na Petro;
Tito katika **2Kor 8:23**, - *mjumbe* katika KJV haswa ni *mtume.*

Yakobo, ndugu wa Bwana katika **Gal 1:19**; nduguze Bwana katika **1Kor 9:5** – wanatajwa katika **Mariko 6:3** kuwa Yakobo, Yose, Yuda na Simoni;

Epafrodito katika **Flp 2:25** – *mjumbe katika KJV haswa ni mtume,* neno sawa la Kiyunani *apostolos.*

Silvanus na Timotheo katika **1The 1:1 na 2:6**.

Ni nani aliyemtuma Paulo kama mtume?

Mdo 13:2-4a inasema Roho Mtakatifu aliwaambia viongozi katika kanisa kule Antiokia ***"Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao. Basi watu hao, wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu…".*** Walitumwa na Roho Mtakatifu lakini Roho Mtakatifu alitumia viongozi waliokusanyika ***"Manabii na waalimu" (*aya 1)** hakika kuwatuma.

Katika **Mdo 14:4 na 14**, Barnaba na Sauli, sasa akiitwa Paulo, wanatabulika kama mitume. Hawaitwi tena nabii na mwalimu, lakini kama mitume. Hawa sio mitume wa mwana kondoo (**Ufu 21:14**). Wanapaswa kuwa tu kumi na wawili, na Mathiya (**Mdo 1:25:26**) akachukua nafasi ya Yuda awe mtume wa kumi na wawili.

Kwa hivyo Paulu na Barnaba ni mitume wa aina gani na wengine waliotabuliwa katika agano jipya? Hao ni mitume kulingana na karama ya huduma za kupaa zilizopatianwa na Yesu alipopaa **(Efe 4:7-12)**. Tambua kwamba karama ya huduma ya mtume hatimaye iliachiliwa kwa wale thenashara wakati Yesu alipaa – walijazwa na nguvu na karama siku ya pentekote, lakini wale kumi na wawili ni spesheli kwa sababu ***"walifuatana na Yesu kuanza tangu ubatizo wa Yohana, hata siku ile alipochukuliwa kwetu kwenda juu"*** **(Mdo 1:21-22).**

Mitume wengine wote wamechaguliwa na Yesu katika kupaa kwake. Kupinga kwamba kuna mitume leo ni kupinga kuwa Yesu amekaa katika enzi.

JUKUMU LA MTUME NI LIPI?

Kujenga nyumba ya Mungu

Tayari imetajwa kwamba jukumu la kwanza ni kuwakilisha na kufanya aliyetumana ajulikane. Kazi au jukumu la mtume kisha ni **kujenga nyumba ya Mungu.** Yesu alitangaza katika **Mt 16:18** kwamba atalijenga kanisa lake. Alikuwa tayari amewachagua mitume kumi na wawili na ni kwa kuwaandaa na kuwatayarisha kwamba Yesu alijua ya kuwa kanisa litawekwa msingi kulingana na mapenzi yake. Kisha katika **kupaa kwake alipatiana huduma tano kujenga kwa niamba yake.**

Kuweka msingi ulio sawa

Paulo anatuambia katika **1Kor 3:10-11** kwamba kama mtume yeye ni '***mkuu wa wajenzi mwenye hekima'*** ambaye anaweza **kuweka msingi ulio sawa –** ambao ni Yesu Kristo – na kuweka sawa mpago wa kujenga ili huduma zingine ziweze kujenga katika msingi huo ulio sawa. Kazi ya kimsingi ya mtume inathibitishwa katika **Efe 2:19-22** ambapo Paulo anasema kwamba nyumba ya Mungu inajengwa juu ya msingi wa mitume na manabii. Hata kama kanisa limepuuza huduma za mitume na manabii kwa karne nyingi, maandiko yako wazi kwamba ni huduma za msingi unaofaa kwa kujenga kanisa.

NEEMA YA MTUME NI GANI?

1. Kuwa baba

Kwanza mtume anatakiwa awe baba, akiwalea watoto wawe wana. Katika **1Kor 4:14-16**, Paulo anaongea na kanisa la Korintho kama "***watoto niwapendao".*** Alisema ***"kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya injili".***

Paulo anawaandikia wagalatia kwa njia hiyo. ***"vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani Yenu"*** **Gal 4:19.** Wagalatia tayari wameokoka na Paulo ndiye amewahubiria. Kama mtume Paulo alichukua jukumu kuwalea aliowazaa katika Kristo. Alikuwa baba kwao na alishugulika kwamba watakomaa katika Kristo.

Mitume tu ndio akina baba katika mwili wa Kristo? La! Wote waliokomaa wanatakiwa wawe akina baba, lakini moja ya dhihirisho ya neema ya kitume ni moyo wa baba, ambayo inawaleta watoto katika ukomavu, wakifanyika akina baba wakati ufaao. Mtume Yohana alitambua vizazi vitatu kanisani katika kila wakati: watoto wadogo, vijana na akina baba (**1Yn 2:12-14**).

2. Kuleta ufunuo

Pili neema katika mitume ni kuleta ufunuo, kufanya siri ijulikane (**Efe 3:2-8**). Paulo anaongea kuhusu neema ambayo Mungu alimpatia kuelewa na kueleza siri ya Kristo na kanisa lake. Anaongea juu ya hii tena katika **Kol 1:25 26a** ***"nimefanywa mhuduma wake, sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize neno la Mungu, siri ile…".***

Oh, jinsi kanisa linahitaji mahubiri sahihi na mafundisho ya neno leo!

Oh, Jinsi tunahitaji kufunuliwa kwa maandiko, sio maoni na mitazamo ya wanadamu!

Oh, jinsi tunahitaji ***"hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele kwa utukufu wetu"*** **1Kor 2:7.**

3. Kuwa mjenzi mkuu

Tatu neema katika mtume inamwezesha mtume kuwa mjenzi mkuu (**1Kor 3:10**), kuwa na maono kujenga kanisa na kuelekeza huduma zingine zifanye kazi pamoja kuleta kanisa katika ukomavu (**Efe 4:12-13**). Tunaporudia muundo wa huduma wa agano jipya, tukiwafanya wanafunzi badala ya kuyajenga makanisa, tunapofuata mfano wa kiutume wa mitume na wandugu katika maandiko tutakuwa ***"wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi*** **(Flp 3:17).**

4. Kutambua mwito wa wengine kwa huduma

Nne neema ya mtume ni kubabanua na kutambua wito juu ya maisha ya watu binafsi kuwa wahuduma; kuwainua katika huduma; na mwisho kuwatuma kufanya kazi ya huduma.

Timotheo katika maandiko ni mfano wa maajabu katika haya. Imenakiliwa katika **Mdo 16** kuwa Timotheo alikuwa mwanafunzi ***"alishuhudiwa vyema na ndugu"*** **(aya 2).** Paulo alitaka Timotheo aende naye, na akafanya hivyo. Paulo alimfundisha Timotheo katika huduma na kwa wakati uliofaa akaweza kumtuma Timotheo aende kwa huduma kama ***"mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana"*** **1Kor 4:17.** Hata wakati Timotheo anafanya kazi kwa uhuru katika huduma, Paulo anamuandikia, akimhimiza ***"uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako"*** **(2 Tim 1:6).**

5. Kupenda kanisa

Tano, neema ya mtume ni kuupenda mwili wa Yesu Kristo. Paulo alipenda kanisa kabisa. Alisema kwa Wakorintho ***"mioyo yetu imekujuliwa"* (2 Kor 6:11)**. Katika pahali pengine anaongea kuhusu mizigo iliyomsukuma ya makanisa aliyoyabeba (**2Kor 11:28**).

Uhakika wa utume!

Neno utume linatumika mara nne katika agano jipya. Ni neno la Kiyunani *apostole*. Neno hili linamaanisha 'tume'. Tunaita maagizo ambayo Yesu aliwapa mitume katika **Mt 28:19-20** tume. Tume ni kuenenda katika mataifa kuwafanya wanafunzi. Tambua kwamba katika kuwafanya wanafunzi, tukiwaleta katika imani na ubatizo ni sehemu ya kwanza katika uwanafunzi; ila hali ulimwenguni kote kanisa linajishugulisha na "kuwafanya watu waokoke" ili waende mbinguni, na wanakosa kuwafundisha neno la Mungu ili wawe wanafunzi waliofaulu katika ulimwengu wakionyesha uhakika wa Kristo na ufalme wake.

1) Wito haswa wa kuwa mtume

Utume umetajwa katika **Mdo 1:25**, na haswa inaonyesha mmoja wa wanafunzi akifanyika 'mtume wa kumi na wawili wa mwana kondoo'. Kwa jumla **utume hapa unaonyesha wito haswa wa mtu kuwa mtume.** Watu wawili walifaulu kufanyika mtume wa kumi na wawili lakini mmoja akachaguliwa – hii ndio ilikuwa hatima yake yenye msingi wa wito wa Mungu na utauwa sio kwa kuhitimu kwa mwanadamu au kuchaguliwa.

Mtu anahitaji kuujua wito haswa na uchaguzi wa kuwa mtume. Paulo alishuhudia kuwa alikuwa **amemwona Bwana!** Wengi wemesema mtume leo anatakiwa awe amemwona Bwana. Wakati jambo hili halijakasiwa katika maandiko, kanuni ni ya muhimu. Wengi wamechanganyikiwa leo kuhusu **mitume ni akina nani**?

Ushuhuda wangu ni kuwa nimemwona Bwana; ninajua kuwa mimi ni mtume kwa wito wake na utauwa. Kwa hivyo maoni ya wengine hainipotoshi. Ukiwa wewe ni mhuduma wa Kristo inakupasa kujua wito wake.

2) Huduma kwa mataifa

Utume umetajwa katika **Rum 1:5**, na hapa Paulo anatwambia kwamba ***"neema na utume"*** ndio njia ambayo mataifa wataletwa katika ***"kujitiisha kwa imani".*** **Neema na utume ndio njia Mungu anapatiana kutimiza tume.**

Tume ni kufanya wanafunzi wa mataifa yote. Tunaweza kuwa na maono ya kuwafikia watu fulani au kuyapanda makanisa mengi sana, lakini Mungu ametutuma kuyafikia mataifa yote kwa kuwafanya wanafunzi na ni kwa neema ambayo anapatiana na kwa karama na huduma ya utume tunawezeshwa kufikia taifa nzima.

Hii haifanyiki kimsingi katika kuihubiri injili wala kwa kuyapanda makanisa lakini ni kwa kuwafanya wanafunzi, ambayo inahusisha kuhubiri, kubatiza na kufundisha. Kufanya wanafunzi ndio njia ya kuongezeka na kwa hivyo kutimiza tume.

Katika Kristo tumepokea neema na utume kufikiya taifa nzima na mataifa yote.

Katika huduma yetu kwa mataifa, vikundi zinapoenda kutoka SHILOH, tunayaona mataifa yakifikiwa. Mfano wa haya imetendeka Kenya. Ndugu aliyekuwa kiongozi mkuu wa ndini kubwa ya kipentekote [makanisa 4000 +] katika taifa hilo alikuja Australia mwisho wa 2006. Katika Australia alikutana na baadhi ya wanafunzi waliompa mojawapo ya vitabu vyangu vinavyo fungua mafundisho ya kitume.

Nilipoenda Kenya '07, aliniuliza nije niwafundishe wachungaji wake mafundisho ya kitume. Tulifanya hivi kama kikundi kwa njia ndogo katika mwaka wa 2007 na kisha 2008 nilitumia majuma mawili na nusu nikitumika na askofu kwa mikutano kadhaa ya wachungaji katika dini hiyo.

Kwa kufundisha kwa uaminifu mafundisho ya mitume, ambayo ni yale yote Yesu aliamuru (**Mt 28:19**) na yale yote Roho Mtakatifu alifunua kwa Paulo na wengine kama ilivyoandikwa katika agano jipya, tunashuhudia mataifa yakifikiwa. Mafundisho ya kitume sio ya dini; hayana vifungo kwa njia yoyote; ni mafundisho yaliyonyooka ya neno la Mungu kama lilivyoandikwa.

3) Tunda la huduma

Utume umetajwa katika **1Kor 9:2**, ***"Ninyi ndinyi muhuri ya utume wangu katika Bwana".*** Hii **inaongea kuhusu tunda la nyumbani la mtume.** Paulo anasema kwamba wandugu wa Korintho ni thibitisho ya utume wake.

Kila mtume ambaye hakika anatumika kama mtume ataweza kuwa na kikundi cha nyumbani au baadhi ya makanisa ambao ni tunda la huduma na kwa hivyo uhakika wa utume. Kisha mtume au mitume au mjumbe wa kitume kama barnaba katika **Mdo 11** akitumwa kwa kanisa mpya katika Antiokia (**aya22**), wanatumwa kutoka kanisa la nyumbani. Kunatakiwa kuwe na mtu wa kutumana na kituo ambacho unatoka!

Utume ni zaidi ya kuwa mhuduma wa kutembea tembea anayefaulu. Kunahitaji kuwa na mazao ya huduma ya mtume kutoka nyumbani na katika huduma [wana] wanaoinuliwa na mtume. Kwa mfano Paulo aliweza kumtuma Timotheo ***"aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakaye wakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo"*** **1Kor 4:17.** Paulo alikuwa na uhakika wa kumtuma Timotheo na kikamilifu kujua kwamba angemwakilisha. Timotheo alikuwa ni tunda la huduma ya Paulo.

Katika kumtuma Onesimo kwa bwana, Filemoni, Paulo alisema, ***"Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu, yaani, Onesimo…niliyemtuma kwako yeye mwenyewe, maana ni moyo wangu hasa"*** **(Filemoni 10-12).** Mabadiliko ya Onesimo ambayo yangeshuhudiwa na Filemoni, ilikuwa ni tunda la huduma ya Paulo.

Paulo anasema kwamba alikuwa ***"mtume wa Yesu Kristo; kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu"*** **Tito 1:1.** Alisema kwa Wakorintho ***"Kwa maana ikiwa mimi si mtume kwa wengine, lakini ni mtume kwenu ninyi"*** **1Kor 9:2.** Kama wewe ni mtume, basi wewe ni mtume kwa nani? Swali hili ni lazima liweze kujibiwa.

4) Maeneo ya huduma

Utume umetajwa katika **Gal 2:8** na hapa **inaongea kuhusu maeneo ya huduma ya mitume fulani.** Petro alitambuliwa kama aliyehusika kuipeleka injili kwa 'waliotahiriwa' na Paulo kwa 'wasiotahiriwa'.

Haya yalikuwa ni maeneo makubwa sana ya majukumu na tunajua kuwa mitume wengine wengi walihusika katika maeneo yote mawili. Tomaso, mmoja wa wale kumi na wawili aliipeleka injili India. Hivi juzi tulikuwa tukihudumu India na tukashuhudia kumbukumbu ya Tomaso ni dhahiri mpaka leo.

Paulo anaongea kuhusu maeneo ya huduma katika **2Kor 10:12-18**. Anaweka alama zilizo za muhimu:

- Hatupaswi kujilinganisha ***"pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe"*** **aya 12**
- Hatupaswi kujipima au kujilinganisha na wengine **aya 12**
- Tunahitaji kujua vipimo au mipaka ya maeneo ya huduma ***"kwa kadili ya kipimo tulichopimiwa na Mungu"*** **aya 13**
- Tunapaswa kujua ni wapi tulio na mamlaka **aya 14**
- Hatupaswi kujisifu ***"zaidi ya kadiri yetu"*** au ***"katika taabu za watu wengine"*** **aya 15a**
- Imani ya wandugu katika maeneo ya mtume inapanua utendaji wa mtume **aya 15b**
- Tunapaswa kuhubiri injili ***"katika nchi zilizo mbele"*** **aya 16a;** ujumbe wa kitume unapaswa kufikia dunia yote.
- ***"tusijisifu katika kipimo cha mtu mwingine kwa mambo yaliyokwisha kutengenezwa"*** **aya 16b.**

Maeneo ya huduma ya mtume ni lazima yaanze mahali. Kwa Paulo ilikuwa atumwe katika safari za umisheni. Alirudi kutoka safari hiyo akiwa amefaulu kuyapanda makanisa na kuwafanya wanafunzi.

Tulipoanza huduma yetu Toowoomba mwanzo wa 1998, tulianza kwa kufundisha neno, kuumega mkate, na kuomba kutoka nyumba kwa nyumba. Kwa muda tukawa na wanafunzi walifanyika sehemu ya huduma. Katikati mwa 2001 kulikuwa na wanafunzi wa kutosha kuunga kikundi cha kitume. Kutoka kituo hiki mie binafsi nimeenda katika mataifa na vikundi na wengine wengi wameenda na vikundi kutoka kikundi cha kitume cha SHILOH kwa mataifa.

Kutoka katikati mwa 1999 tumeweza kuimarisha shule za muda mfupi na sasa tuna shule ya kitume inayofanya kazi.

Kuna mpango

Kanisa haliwezi kujengwa bila mitume wanaofanya kazi. Paulo alisema, ***"kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake"*** **1Kor 3:10.** Mfano wa kanisa tunaloliona leo ni moja ya utatanishi. Kila kiongozi wa kanisa, wakihusisha wachungaji wa dini, wanajenga kulingana na maono yao, kwa matakwa yao. Hawajihusishi na mtume; hawajafundishwa katika mafundisho ya kitume na ufahamu wa neno la Mungu; na kwa hivyo kanisa linajengwa katika njia yoyote, pasina kuliwakilisha kanisa la maandiko na kukosa kuonyesha utukufu wa Mungu.

Ni ya huhimu kuwaelewa mitume, huduma ya mtume na utume katika siku hizi za urejesho. Wengi wanaitwa mitume au wanajiita mitume siku hizi. Wengi wanajiuliza tutajuaje ni nani aliye mtume? Natumai kwamba mafundisho haya mafupi yanatusaindia kutambua na kupokea karama ya huduma ya mtume, ambayo Kristo ameweka kanisani.

THIOLOGIA YA KITUME
[ELIMU YA KITUME]

Ukosefu wa maarifa ya Biblia

Nikirudi kutoka Asia katika March '08, ambapo nilikuwa nimefundisha katika mkutano wa wachungaji na viongozi Myanmar na India kwa mwezi mmoja, niliguzwa na kuona ukosefu wa maarifa ya biblia. Wengi wa wandugu waliokusanyika walikuwa na Degree katika Theologia, wengine wakiwa na Masters na Doctorates. Hata hivyo, pasina kujali Shahada walizokuwa nazo kulioneka kuna hoja kubwa ya kutoelewa maandiko 'kama ilivyoandikwa'.

Niliona vyema kuwauliza wajumbe wa kongamano wakubaliane nami katika mwanzo wa kongamano kwamba mtazamo wa msinigi wa imani ni kuamini kwamba **"maandiko ndio mamlaka yetu tu ya imani na utendaji"** na kuwa ***"kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki"*** **2Tim 3:16.**

Theologia

Neno *Theology* inatoka kwa majina mawili ya Kiyunani: *Theos* ikimaanisha *Mungu* na *Logos* ikimaanisha *neno*. Tukiongea kwa kumaanisha, thiologia inapaswa kuwa ni mafundisho ya neno la Mungu. Hata hivyo nidhamu ya ndani na shule za elimu ya mawazo zimetokea kwa karne nyingi na wengi wanaohudhuria Chuo cha Biblia au Seminari wanafundiswa kulingana na moja wapo wa shule hizi kuliko kufundishwa neno kama lilivyoandikwa.

Katika kuangalia thiologia ya kitume, ninamaanisha kurudi kwa maandiko kikamilifu kama ilivyoandikwa, kufahamu mazingira na kulitumia neno kama mitume katika agano jipya walivyofanya.

Kanuni ya maandiko

Maandiko yamekamilika! Hii ilikubalianwa katika mwanzo wa majira ya kanisa na wanaohusika katika kuziweka kanuni za agano jipya walipokea msukumo wa kushangaza na uthibitisho wa Roho Mtakatifu kubeba wajibu huu muhimu. Ni ya kimsingi kwetu kukubali kanuni ya maandiko, agano la kale na lile jipya, sio kuongeza wala kupunguza kilichoandikwa.

Ni lazima tuwe makini sana tunapotoa utafsiri wa maandiko na kufundisha 'ufunuo' wetu wa kivuri na mifano katika agano la kale. **'Hapo mwanzo kulikuwako neno, sio utafsiri'**

KANUNI SABA ZA THEOLOGIA YA BIBLIA – JINSI YA KUSOMA NA KUTAFSIRI MAANDIKO:

1. Biblia ni neno la Mungu

"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu" **2Tim 3:16.**
"Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" **2Pet 1:21.**

Msingi katika kujifundisha kwetu ya neno la Mungu ni kukubali kuwa **biblia ni neno la Mungu.** Kuna dini Australia ambayo imeandika katika msingi wa imani yao kuwa 'biblia ina neno la Mungu'. Katika hali ya dini hiyo sasa wanaidhinisha kuwekwa wakfu kwa usoga.

Yesu alishinda majaribu ya shetani kwa kujua 'ni nini kilichoandikwa' (**Mt4:1-11, Lk 4:1-14).**

Yesu anaiweka wazi kuwa neno la Mungu ni hakimu wetu (**Yn 12:48**). Yesu aliweka wazi kwamba hakuyanena maneno yake lakini amri ya Baba, ***"kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo"*** **Yn 12:49-50.**

Paulo ana uhakika kwamba ***"mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe"*** **1Kor 4:6.** Mamlaka yetu tu ya imani na utendaji ni neno la Mungu. Tunapoenda zaidi ya hayo, hatuna ***"timanzi"*** ya kutegemewa ya kuamua kutegemea tunayoshirikishwa.

"Nao wataiona timanzi katika mkono wa Zerubabeli; naam, hizi saba [ikiongea kuhusu Roho Mtakatifu***] ndizo macho ya BWANA; yapiga mbio huko na huko duniani mwote"*** **Zakaria 4:10**. Zerubabeli ni mfano wa mtume; jukumu lake lilikuwa ni kujenga nyumba ya Mungu. Jukumu la msingi la mtume ni kujenga nyumba ya Mungu. Timanzi ni "***neno la YAHWEH kwa Zerubabeli"*** **aya 6.** Kwa hivyo tunapaswa kuamriwa na kuamua mambo yote kupitia neno la Bwana Yesu kama inavyokuja kupitia mitume wake (**2 Pet 3:2),** na kama *neno lililohuishwa* linakuja kwa kila mmoja wetu (**Rum 10:17).**

2. Agano Jipya linapatikana katika Agano la Kale; Agano la Kale limetimizwa katika Agano Jipya

"*Akaanza kutoka Musa na Manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe"* **Lk 24:27.** Yesu alikuwa tu na maandiko ya Agano ya kale kama ilivyokuwa na mitume wa kwanza, lakini waliweza kuhubiri injili kwa nguvu kutoka Agano la Kale.

"*Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa, na katika Manabii, na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko"* **Luka 24:44-45.**

Funguo ni kupata ufahamu wetu ufunguliwe. Ombi la Paulo katika **Efe 1:17-18** ni funguo kwetu: omba Mungu kwa roho wa hekima na ufunuo na kwa ufahamu wetu ufunuliwe tumjue Kristo katika Agano Jipya na la Kale.

"***Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini"*** **Rum15:4.**

"Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani" **1 Kor10:11.** Maandiko ya Agano la Kale yapo kutuelekeza katika saburi na faraja, ikituleta katika tumaini lililo hai katika Kristo katika miisho ya zamani.

"Injili ya Mungu; ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu" **Rum1:1-2.** Kufahamu injili, tunapaswa kufahamu mafundisho na ahadi za Mungu kutoka kitabu cha **mwanzo** mpaka **malaki,** na kuona kwamba ahadi hizo na mafundisho hayo yametimizwa katika agano jipya.

Filipo alihubiri yesu katika kitabu cha Isaya (**Mdo 8:30-35**). Alihubiri na kufanikiwa sana kwamba mtu wa Kushi akauliza abatizwe mara moja.

Kitabu cha **Waebrania** ni tafsiri ya ajabu ya Agano la Kale ikionyesha kutimizwa kwa Agano la Kale katika Yesu Kristo na kwa hivyo Agano la kale limetimizwa katika Jipya.

3. Linganisha andiko na andiko

Mafundisho ya Biblia katika fundisho lolote ni mkusanyiko wa yale yote Biblia inasema kuhusu fundisho hilo. Kupitia kutumia Concordance tunaweza kufanya mafundisho ya maneno, tabia, maeneo ama vichwa katika biblia. Tunaweza kutafuta kile biblia inasema kuhusu fundisho fulani na kuhubiri na kufundisha neno la Mungu na mamlaka.

Tabia ya Henoko, mwana wa Yaredi, ni mfano mndogo wa kulinganisha andiko na andiko. Henoko anatajwa kwanza katika **Mwanzo 5:18-24;** anatajwa katika ukoo wa Yesu katika **Luka 3:37**. Kisha tuna tafsiri kamili [kutimizwa] katika **Waebrania 11:5-6**, na kutajwa kwingine ni katika **Yuda14-15**, ambapo Henoko anaonekana kama nabii na akipata maono ya kuja kwa Kristo mara ya pili. Kutoka kwa kutajwa huku kuchache kwa mtu Henoko, wa saba kutoka Ibrahimu [asifananishwe na Henoko mwana wa Kaini], tunaweza kuhubiri na kufundisha ujumbe wa maajabu kuhusu kutukuzwa kwa kanisa.

4. Andiko linatafsiri andiko

Kujaribiwa kwa wanafunzi wa Biblia ni kukimbia kuangalia wanaotoa maoni na yale wasomi wa Biblia wamesema kuhusu maandiko au kwa wepesi kuamini mafundisho ambayo mtu amefundishwa ambayo hayatoshi kuthibiti kujaribiwa kwa mamlaka utafsiri wa kweli wa maandiko [hii inaitwa hermeneutics].

Baadhi ya mifano ya andiko likitafsiri andiko:

Katika **Ufunuo1:20,** Yesu anatafsiri nyota na kinara. Kwa sababu ya aya hii ya kutafsiri tunaweza basi kuelewa mfano wa kinara katika hema ya Musa, na katika **Zakaria 4**, na tunapokea msaada kuelewa **Ufunuo 11:4** ambayo inatambua wale mashahidi wawili kama ***"vinara viwili".***

Katika **Yohana 3:5-6**, Yesu anatafsiri ***maji*** kama kuzaliwa ***upya*** au kuzaliwa kwa asili. Hatuhitaji utafsiri mwingine zaidi wa maji katika mazingira haya!

Katika **Mathayo 13,** Yesu anatafsiri mifano miwili neno kwa neno. Kwa hivyo tuna mamlaka ya utafsiri kutoka kwa maandiko wa mifano hiyo.

5. Fundisha na utafsiri andiko katika mazingira

Kila aya ya biblia inapatikana katika **kifungo** kwa hivyo hayo ndiyo mazingira ya kwanza; kila kifungo kiko kwa **sura**; kila sura iko katika **kitabu**. Kila kitabu kinapatikana katika **agano** na mwisho kifungo chote kikamilifu kiko katika **Biblia yote.** Mtu mmoja amesema: *kifungo bila mazingira ni cha uongo!* Kila fundisho la kizushi lililotolewa katika biblia inatokana na kuondoa kifungo kwa mazingira na kufanya mafundisho ya vitengo vya dini.

Wanawake katika huduma – mwanamke anatakiwa kufundisha au hata kuongea?

Mfano katika kanuni ya mazingira haya katika mazingira ya Biblia yote 'ni huduma ya wanawake'. Wengi wamefanya makosa ya kuchukua **1Tim 2:11-12** kama amri ya kuwa wanawake hawastahili kuwafundisha wanaume lakini ***"awe katika utulivu",*** kwa hivyo hata wasiruhusiwe kuongea katika mikutano ya kanisa. Hata kifungo chenyewe kinaongea juu ya ***"mwanamke"*** na haiongei juu ya wanawake kwa jumla.

Katika mazingira ya kifungo mwanamke fulani anafananishwa na Hawa ambaye alichukua sehemu ya mumewe kwa nguvu na akamuelekeza kuyapokea mafundisho ya uongo.

Katika mazingira ya sura Paulo tayari amepeana maagizo kwa wake na waume ***"wazalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyo takata"*** **aya 8-10.** Katika **aya 10** anaongea

juu ya ***"wanawake wanao ukili uchaji wa Mungu"*;** kutangaza inamaanisha kukiri na kwa hivyo wanawake wanatarajiwa kuongea kuhusu imani yao kwa yeyote.

Katika mazingira ya barua za Paulo kwa **Timotheo**, kuna kutajwa kwa mama na bibi yake Timotheo wote wakihusika katika kushiriki na kufundisha maandiko na imani kwa Timotheo (**2Tim 1:5, 3:15).**

Katika vitabu vingine vilivyoandikwa na Paulo anawataja wanawake ***"asalipo au anapohutubu"* (1Kor 11:5)** na katika **Tito**, wanawake wanapaswa wawe ***"wafundishao mema"* (2:3).**

Katika mazingira ya Agano Jipya, hakuna anayepinga mwanamke wa Samaria akiwashuhudia wanaume katika jiji lake (**Yn 4**).

Katika mazingira ya Biblia yote, Mungu mwenyewe alimchagua Debora awe mwamuzi wa Israeli (**Waamuzi 4:4**), pia nabii mke na ***"mama katika Israeli"* (Waamuzi 5:7).**

6. Usiweke uzito katika mambo madogo

Paulo alimwambia Timotheo ***"wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani"* 1Tim 1:4.** Wengi wanataka kubishana na kuweka sheria ya wanawake kufunika vichwa. Katika mazungumzo ya Paulo katika **1Kor 11:2-16**, Paulo hatimaye anasema ni ***tamaduni tu.***

Tunahitaji kufundisha na kuhubiri ***"yote niliyo waamuru [Yesu] ninyi"* Mat 28:20.** Tunahitaji ***"kunena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima"* Tito 2:1.** Tusitengeneze ujumbe juu ya mawe matano ambayo Daudi alibeba katika mkoba wake kupigana na Goliathi. Sio kitu cha kufananisha na huduma tano au kitu kama hicho.

7. Uliza maswali yako ya maandiko na ugonje jawabu za maandiko

Kwa mfano katika **Habakuki 2:1-3,** nabii aliandika maono lakini ilibidi angojee yatimizwe.

Baadhi ya 'wahubiri wa siku za mwisho' wametumia vichwa vya magazeti na historia ya kisasa kujibu maswali ya Biblia na waamini wamepokea mawazo hayo, wakishawishika kuwa ni maandiko. Hata Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa hakujua ***"siku ile na saa ile"* (Mt 24:36).** Tunapaswa kujihadhali jinsi gani kabla ya kutangaza utafsiri wa yaliyonenwa katika biblia kwa kile tunaita unabii wa 'siku za mwisho'.

Biblia ina jawabu zote na Biblia itajijibu.

Jia ya msaada ya kuangalia agano jipya kwa jumla

- Katika injili Yesu anatuambia cha kufanya: ***"yote niliyowaamuru ninyi"* Mat 28:20.**
- Katika kitabu cha matendo, mitume wanatuonyesha jinsi ya kuifanya, hivyo ni, jinsi ya kuzitii amri za Yesu.
- Katika nyaraka mitume wanaeleza ama kufundisha kwa nini tunayafanya yale yameonyeshwa katika kitabu cha Matendo ya mitume.
- Katika kitabu cha ufunuo kuna kutimizwa kwa mambo yote katika Masihi Yesu.

Mfano ni ubatizo

i. Yesu aliamuru ubatizo katika **Mathayo 28:19** na **Mariko 16:16**.

ii. Mitume walitii Yesu kwa kubatiza wote waliokuja kwa imani ndani yake. Mitume walituonyesha jinsi ya kubatiza katika kutii maagizo ya Yesu.
Yesu alisema tubatize ***"kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu".***
Petro aliwaamuru ***"wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo"* Mdo 2:38.**

Katika Samaria waamini wapya walibatizwa ***"kwa jina lake Bwana Yesu"*** **Mdo 8:16.** Filipo alikuwa amefundiswa na mitume kule Yerusalemu.

Yule mlinzi wa gereza alibatizwa katika msingi wa ***"kumwamini Bwana Yesu"*** **Mdo 16:31, 33.**

Paulo aliwabatiza tena wanafunzi wa Yohana ***"Kwa jina la Bwana Yesu"*** **Mdo 19:5.**

iii. Katika nyaraka tunafundishwa mafundisho ya ubatizo, hivyo ni, maelezo au sababu tunabatizwa.

Katika **Rum 6:3-14**, Paulo anafundisha kwamba tunabatizwa katika mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo. Bila ubatizo wa maji, tuko kikamilifu ndani ya Yesu?

Katika **1Pet 3:21-22**, Petro anathibitisha kwamba tunabatizwa katika kufufuka kwa Yesu Kristo.

iv. Kuhusu utimilifu katika kitabu cha **ufunuo**, kuna ***"mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana kondoo"*** **Ufu 7:9.** Hawa ni waamini wa kweli ambao wamebatizwa ndani ya Yesu Kristo. Wako na umoja na yeye.

Hebu turejelee thiologia ya kitume

Wengi ambao wamekubali wito wa huduma ya neno wamefundishwa vibaya kwa huduma hiyo, na wengi wa hawa wameongozwa kujitolea kukubwa ili wahudhulie vyuo vya biblia au seminari. Wanatumia dola ambayo ni vigumu sana kuchanga ili wajipatie vyeti au diploma au degree au hata degree ya juu; ilahali wanachohitaji ni mwalimu wa Biblia ambaye amefundishwa vizuri ambaye amekubatia na kufahamu kikamilifu mafundisho ya kitume.

Kupitia kuhubiri na kufundisha ukweli wa neno la Mungu, wahuduma wanaweza kufundishwa kufanyika ***"wahubiri, mitume na waalimu wa mataifa katika imani na kweli"*** **(1Tim 2:7).**

Tunapaswa kutafuta ukweli! Tunastahili kujifundisha kwa imani na katika imani! Hatupaswi kuzihudhuria idara kwa faida ya kupewa karatasi. **Ni wakati wa kurejelea thiologia ya kitume.**

Msemo huu ulinenwa kwangu katika chuo cha Biblia katika Yangon, Myanmar. Nilikuwa nimekaribishwa ili niweze kuongoza katika kufuzu wanafunzi wa Bachelors na Masters. Nilikubali kufanya haya kama ningeruhusiwa kuwafundisha wanafunzi hao waliokuwa wakifuzu kwa siku tatu. Katika mamkuli ya mchana siku ya pili, Yule Rev. Dr. aliyekuwa mkurugenzi mkuu wa chuo alisema kwangu, 'ndugu Paulo, sisi tumekuwa na thiologia ya mpangilio katika chuo hiki lakini hatujakuwa na Thiologia ya Kitume hapo mbele'. Walikuwa wamesikia nini? Walikuwa wakisikia maandiko yakifunguliwa kama yalivyoandikwa, mstari kwa mstari, aya kwa aya. Walishangaa kwa sababu mengi yapo ya mafundisho walioyapenda yalionekana kuwa hayana msingi wa maandiko.

Thiologia ya kitume ni kulieleza neno la Mungu kama lilivyoandikwa; kumhubiri Kristo ***"tukimuonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo".*** **Kol 1:28.**